Kesi

Kwa ajili ya kusoma Maandiko, alasiri ya leo, kutoka kwenye Kitabu cha Marko, mlango wa 16 wa Marko. Nami ninawatakeni msimame, pamoja na Biblia zenu, tunapolisoma Neno la Mungu. Marko 16, kuanzia kifungu cha 9.

> *Naye Yesu alipofufuka alfajiri siku ya kwanza ya juma, alimtokea kwanza Mariamu Magdalene, ambaye kwamba alimtoa pepo saba.*
>
> *Huyo akashika njia akawapasha habari wale waliokuwa pamoja naye, nao wakali wanaomboleza na kulia.*
>
> *Walakini hao waliposikia kama yu hai, naye amemwona, hawakusadiki.*
>
> *Baada ya hayo akawatokea* kwa sura nyingine, wawili . . .(Samahani.)
>
> *Baada ya hayo akawatokea watu wawili miongoni mwao, ana sura nyingine; nao walikuwa wakishika njia kwenda shamba.*
>
> *Na hao wakaenda zao wakawapasha habari wale wengine; wala hao hawakusadiki . . .*
>
> Baadaye, *akaonekana na wale kumi na mmoja walipokuwa wakila, akawakemea kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, kwa kuwa hawakuwasadiki wale waliomwona alipofufuka katika wafu.*

2 Hiyo si ni picha ya siku hizi! Hawaamini wewe ni shahidi wa jambo hilo.

> *Akawaambia, Enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe.*
>
> *Aaminiye na kubatizwa ataokoka; asiyeamini, atahukumiwa.*

3 Hilo linafanya tu mpaka, upande mmoja ama mwingine.

> *Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya;*
>
> *Watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono* yao *juu ya wagonjwa, . . .watapata afya.*
>
> *Basi Bwana, baada ya kusema nao, akachukuliwa juu mbinguni, akaketi mkono wa kuume wa Mungu.*

*Nao wale wakatoka,. . .*wakahubiri *kotekote. Bwana akitenda kazi pamoja nao,. . .kulithibitisha lile neno kwa ishara zilizofuatana nalo. Amina.*

Na tuinamishe vichwa vyetu.

4 Bwana, tunaamini hili kuwa ndilo agizo la mwisho kwa kanisa. Tunaamini ya kwamba Neno lilifanyika mwili likakaa miongoni mwetu. Na tunaamini kwamba mtu yeyote si bora kuliko neno lake, kwa hiyo tunaamini ya kwamba Neno hili ni Wewe. Nasi tunaamini ya kwamba ni Wewe, ambapo, ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Njoo, leo, Ee Baba Mungu, katika umbo la Neno, kwetu, na uwajalie watu waone ya kwamba Wewe Ndiye Kristo aliyefufuka, na umefufuka katika siku hii ya mwisho, katika umbo ulilosema ungekuwa ndani yake, Neno lililodhihirishwa. Ulipokuwa duniani, Wewe ulikuwa Ndiye Neno lililotabiriwa, lililodhihirishwa katika umbo la mwanadamu. Nalo Neno limetabiriwa kwa ajili ya siku hii. Njoo, Bwana Yesu, na utuletee Hilo, leo, lile Neno. Toa tafsiri Yako ya Neno, tupate kuwa na "furaha isiyoneneka, na iliyojaa utukufu." Kwa kiasi kwamba tumekuona U wa kupendeza, na tukayaona Maneno Yako kwamba ni ya kweli na yakathibitishwa mioyoni mwetu, kwamba tumepita kutoka mautini kuingia Uzimani.

5 Sisi sote tuliozaliwa kwa ule mti mmoja katika bustani ya Edeni, uliokatazwa kuguswa, yule mwanamke, kwa kuwa ndani yake hamna uzima; yeye ni yai tu. Uzima hutokana na Mwanamume, ambaye ni Kristo. Nasi tumezaliwa na mwanamke, na, kama Biblia inavyotwambia, "wa siku chache, na zimejaa huzuni na taabu."

6 Baba, pia tumezaliwa kwa Mtoa-Uzima, kutoka kwa yule Mwanamume. Mtu mume humjia mtu mke, nayo chembe hai inatokana na mume; kama vile Roho Wako alivyomtia uvuli yule bikira, na ndani ya tumbo lake la uzazi ikaumbwa chembechembe ya Damu; hiyo chembechembe ya Damu, si ya Kiyahudi, si ya Kimataifa, bali ni ya Mungu, Damu iliyoumbwa. Katika Damu hiyo, tunayo matumaini yetu. Haikuwa ni ya mwanamke, wala ya mwanamume; ilikuwa ni ya Mungu.

7 Kwa hiyo tunaomba leo hii, Bwana, kwa kuwa tumejiona wenyewe ni washiriki wa ule mti-mwanamke, nasi sote hatuna budi kufa kwa sababu hamna uhai katika mwanamke, sasa pia, Baba, tumepewa majaliwa ya kushiriki kwenye ule Mti-Mume, ambao ni Kristo. Na sasa, kupitia Yeye, tunao Uzima, Uzima, lile Neno, limekuwa Uzima miongoni mwetu. Tujalie, Bwana, ya kwamba mambo haya yatakuwa halisi sana kwa Kanisa, hata wataona, nasi tutafahamu ile saa tunayoishi.

8 Waponye wagonjwa na wanaoteseka. Jalia pasiwepo na mtu aliye mnyonge miongoni mwetu, alasiri ya leo, hapo ibada hii itakapoisha. Jalia ikumbukwe kwa muda mrefu sana miongoni mwa watu! Wajalie watumishi Wako, wa—wachungaji,

wachunga kondoo, jalia wavuviwe sana mpaka makanisa yao yatafanyiwa mapinduzi na ibada kuu zifanyike, na waanzishe uamsho wa mtindo wa kale mumu humu katika mji huu, miongoni mwao, ambao utaenea kote jimboni na nchini, na hata kote ulimwenguni. Tujalie, Bwana. Unashikilia funguo za maombi haya mkononi Mwako. Tusaidie, tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

9 Mungu hana budi kuleta hukumu juu ya dunia hii. Naye Mungu hana budi kuwa na kitu fulani hapa, kigezo, kuuhukumia ulimwengu, kwa maana ingekuwa si haki, katika Mungu, kuuhukumu ulimwengu, huku ulimwengu haujui kigezo cha kutumia. Ni wangapi wanaoamini hiyo ni kweli? Kama kanisa ndilo kigezo, ni lipi? Neno, Mungu alisema atauhukumu ulimwengu kwa Yesu Kristo. Yeye ni Neno. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Huyo Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Neno alifanyika mwili akakaa miongoni mwetu." "Yeye yule jana, leo, na hata milele."

10 Sasa ninataka kunena nanyi alasiri ya leo juu ya somo la kigeni sana, huenda likawa hivyo kwenu. Lakini, katika somo hili, nitamfanyia Bwana wangu ke—kesi ya haki. Sidhani alifanyiwa kesi ifaayo mbele ya mahakama ya Pilato. Si—siamini alikuwa na—alikuwa na kesi ya haki, kwa hiyo walimpata na hatia, na wakamhukumu na kumsulibisha. Lakini tutafanya mchezo wa kuigiza, alasiri ya leo, katika kesi hii.

Nanyi mnasema, "Ati ungeweza kumfanyia kesi?"

11 Kama Yeye anadumu akiwa ni Neno, tunaweza kumfanyia kesi, kwa kuwa Yeye angali ni Neno. Nasi tunaweza kumfanyia kesi. Nami ninataka kuona hilo katika mahakama hii, alasiri ya leo, tunapolichukua jengo hili kuwakilisha mahakama, ambapo tunataka kuhakikisha ya kwamba Yeye anapata kesi ya haki, kama ni wanaomtetea ama wanaomshtaki. Tunataka kutoa pande zote mbili. Halafu basi, katika kesi hii, ninataka kuisikiliza kesi Yake, ambaye ni Neno.

12 Sasa, haya Maandiko ambayo ndiyo kwanza nisome, Marko mlango wa 16, hata Daktari Scofield hapa anasema, "Kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, hayapatikani katika magombo mawili yaliyo ya kale zaidi." Inaaminiwa sana miongoni mwa watu, ya kwamba, walimu wetu wa siku hizi wanaotaka kuliamini namna hiyo, ya kwamba yameingizwa mle na Vatikani.

13 Lakini ninaona ya kwamba Ireneo na wengi wa waandishi wa mwanzoni wanarejea kwenye Marko 16. Kama vile ninyi watu wengine mnaoisoma historia, historia ya Biblia, mjuavyo ya kwamba hao mitume wa mwanzoni, na hata baada ya kifo cha Yesu, na wakati Polycarp, na Ireneo, na Mtakatifu Martin, na Mtakatifu Columbas, na wote hao, walirejea kwenye hii

Marko 16. Kwa hiyo hapana budi ilikuwa ni ya kweli, la sivyo wasingaliirejea kamwe. Naye Yohana Mtakatifu ndiye aliyeziweka zile nyaraka pamoja, naye Polycarp alikuwa rafiki msiri na alimsadia kufanya hivyo, kulingana na historia.

14 Sasa tunaona ya kwamba leo hii hawaamini hilo. Wanajaribu kuuondokea uhalisi wa Mungu kuwa ni halisi; badala yake, azimio tu ama kanuni za imani. Mungu aliye halisi, mlango huu ungethibitisha kwamba ni halisi, na thibitisho lolote wanaloweza kulipata.

15 Kama vile mwalimu fulani mashuhuri sana, rais wa Misheni za Sudan, maskini mke wangu pale alikuwapo wakati alipokuja nyumbani kwangu, Paris Reidhead. Naye akasema, "Ndugu Branham, ninasikia ya kwamba ulikuwa Mbaptisti."

Nikasema, "Naam, bwana, hiyo ni kweli."

16 Naye akasema, "Vema," kasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani." Akasema, "Nilipokuwa mvulana mdogo," kasema, "nilipata tukio. Naye mama yangu alifua na kila kitu, apate kunipeleka shuleni. Nami nikawazia, hakika, kwamba nilipopata B.A. yangu, kwamba ningempata Kristo." Akasema, "Hiyo, wakati nilipokabidhiwa hiyo, sikumpata. Nilipopata Digrii yangu ya Udaktari, nilifikiri ningempata. Nilipopata LLD yangu, nilifikiri ningempata." Akasema, "Ndugu Branham, ninazo digrii za kutosha, za kawaida na—za kawaida na za heshima pia, hata ningeweza kukandika kuta zako kwazo. Lakini yuko wapi Mungu wa Biblia?" Akasema, "Hivi walimu walikosea?"

Nikasema, "Mimi ni nani kusema ya kwamba walimu walikosea?"

17 Akasema, "Vema, hivi ndivyo ninavyosikia, ya kwamba uligeuka ukawa Mpentekoste."

18 Nami nikasema, "Vema, sisemi mimi . . . Ninaamini, wakati nilipozaliwa katika Ufalme wa Mungu, moja kwa moja nilifanyika mpentekoste," nikasema, "kwa maana pentekoste si dhehebu. Wamejaribu kuifanya hivyo, bali sivyo ilivyo. Mungu atamjaza Mpresbiteri, Mlutheri, ama yeyote yule uliye. Mnaona, kwa hiyo ni tukio wala si dhehebu. Huwezi kuiundia dhehebu. Ni tukio."

19 Naye akasema, "Vema, ninataka kukwambia kile kilichotukia." Akasema, "Kutoka India, siku hizi, wanawatuma watu huku wapate elimu yao." Kasema, "Shuleni mwetu, kulikuwako na mvulana mzuri wa Kihindi aliyekuja huku na akasomea huku. Ndipo aliporudi . . . " Nafikiri alikuwa awe, nafikiri, mhandisi wa umeme ama kitu fulani. Akasema, "Lakini wakati tuliponinii . . . "

20 Wao wana shule kama tu vile Ndugu Oral Roberts alivyo nayo kule juu. Wanafundisha uhandisi na kadhalika.

21 Kwa hiyo akasema, "Alipokuwa akirudi, mimi pamoja na mhudumu mwingine, tulimwambia, 'Sasa, unarudi India . . .'" Nanyi mwajua Wa—Wahindi wanamwabudu Mohammed. Basi akasema, "'Kwa nini usimwache maskini nabii wako wa kale aliyekufa, na kumpokea Bwana Yesu aliyefufuka; nawe urudi India pamoja na Mungu aliye halisi, ukawaambie watu wako?'"

22 Akasema, "Bwana," akasema, "Bwana wako Yesu angeweza kunitendea yapi zaidi ya yale nabii wangu awezayo kufanya?"

23 Naye akasema, "Vema, Bwana wangu Yesu anaweza kukupa Uzima wa Milele. Ni ahadi katika Neno."

24 Akasema, "Nabii wangu, Muhammed, aliahidi jambo lile lile, kwenye neno lake."

25 Ndipo akasema, "Vema, unaona," akasema, "Bwana wangu Yesu alifufuka katika wafu. Nabii wako yumo kaburini."

26 Akasema, "Ati alifufuka katika wafu?" Kasema, "Mmekuwa na miaka elfu mbili kuthibitisha hilo, na asilimia themanini ya ulimwengu kamwe haijasikia habari Zake." Kasema, "Acha Muhammed afufuke katika wafu, na ulimwengu mzima utajua, katika saa ishirini na nne."

27 Sasa, yeye akasema, "Vema, angalia," akasema, "Yesu amefufuka katika wafu." Kasema, "Ninaweza kulithibitisha kwa kuwa Yeye anaishi moyoni mwangu," kasema huyo Mkristo.

28 Basi huyo Mwislamu akasema, "Pia, bwana, Muhammed anaishi moyoni mwangu."

Akasema, "Lakini, unaona, tuna nguvu na furaha."

29 Akasema, "Bwana, dini ya Uislamu inaweza kutoa saikolojia nyingi tu kadiri Ukristo unavyoweza." Na hiyo ni kweli.

30 Nimewaona wakilala mtaani na kusema kwa sauti kuu, "Allah," na kuingia katika hali fulani, wangeweza kuchukua . . . Mimi na Billy tulisimama tukamwangalia mtu akiuchomeka upanga moja kwa moja chini ya moyo wake; naye daktari akaenda pale na kumwaga maji kupitia hapo, yakatokea upande mwingine; akauchomoa, wala haukumdhuru. Tukawaona wakichukua vibanzi, na kuviweka chini ya makucha yao ya mikono na kuitoboa, na kuchoma ndoana kupitia pua yao, wala wasizihisi wala kutoa hata tone la damu. Wanaweza kutoa saikolojia nyingi zaidi kuliko Ukristo unavyoweza.

31 Ndipo Bw. Reidhead akaniambia, kasema, "Nikajua sikuwa nikizungumza na mshamba. Naye akasema, 'Sisi Waislamu tunangojea.'"

32 Kama walivyomfanyia ndugu yetu shujaa, Billy Graham, mliisoma gazetini, wakati Mwislamu alipomjia Bw. Graham, na kusema, "Wewe wachukue watu thelathini wagonjwa, nami nitawachukua watu thelathini wagonjwa; nawe hebu uwaponye

hao thelathini wako, nami nitawaponya wangu thelathini kwa Muhammed," mnaona, Bw. Graham akatoweka. Asingemjibu.

33 Siamini ningalifanya hivyo. Ningalikuwa kama wale wana wa Kiebrania, "Mungu wetu anaweza kutuokoa na hii." Kwa nini hakutuma, amlete Oral Roberts ama mtu fulani? Kama hakuamini Hilo, aagize aletwe mtu anayeliamini. Lakini, unaona, kwa madhehebu, loo, wangalimtupa nje papo hapo. Yeye ana kazi ya kufanya.

34 Hata hivyo, basi akasema, "Wakati sisi, huko India, tutakapowaona ninyi—ninyi Wakristo mkifanya kile Yesu alisema mngefanya," kasema, "basi tutawaamini." Akasema, "Yeye alisema alifufuka katika wafu, nao watu wangejua hilo kwa sababu mngefanya kazi zile zile alizofanya."

"Vema," akasema, "tunafanya kazi kubwa zaidi."

35 Akasema, "Kamwe sikusema 'kubwa zaidi.' Ninataka tu kuona kazi alizofanya, kwanza." Mbona, unazungumza, unajua huzungumzi na jamaa mdogo huko pembeni, wakati unapozungumza na mmoja wa hao wanatheo-. . .hao pamoja na theolojia yao. Kwa hiyo akasema, "Tunataka kuona kazi alizofanya."

"Loo," akasema, "labda unarejea kwenye Marko 16?"

36 Akasema, "Naam, bwana. Hiyo ni mojawapo, agizo Lake la mwisho kwa kanisa."

37 Akasema, "Vema, sasa, unaona," kasema, "watu wengi wanaamini mlango huo kiulokole." Akasema, "Lakini tulijifunza, wasomi bora shuleni, ya kwamba Marko 16, kutoka kifungu cha 9 na kuendelea, kweli haujavuviwa."

38 Akasema, "Mbona, Bw. Reidhead!" Akasema, "Ni sehemu gani iliyovuviwa basi?" Akasema, "Labda nyingine yote haijavuviwa. Kurani yote imevuviwa. Kwani mnasoma kitabu cha aina gani, kinachoitwa Biblia?"

39 Akasema, "Nimeamua moyoni mwangu nitakuja kuzungumza na wewe. Naam, nilikuwa nizungumze na wewe."

40 Haya basi. Kama *Huu* haujavuviwa, basi vipi kuhusu mingine yote?

41 Inanikumbusha juu ya mama mmoja huko Chicago. Mvulana wake aliondoka akaenda kwenye seminari moja, akasome awe mhudumu, shule fulani ya Biblia na seminari. Basi akiisha kuondoka, mama yake mkongwe akaugua sana. Na kwa hiyo wakatuma taarifa kwa mvulana huyo 'akae chonjo,' mama yake ana homa kali sana, alikuwa na nimonia, na ikasema kwamba (mama) hu—huenda ikawa ni wito wa dharura. Kwa hiyo mvulana huyo akapanga nguo zake na akawa tayari. Hatimaye, kesho yake, hakupata habari yoyote usiku kucha, na kesho yake, kasema, "Yote ni shwari."

42 Kwa hiyo yapata mwaka mmoja baadaye, alirudi kutoka shuleni huko Mashariki, shule kuu ya kufundishia. Basi akaja nyumbani na kumwamkua mama yake wa thamani, na kusema, baada ya kuzungumza kwa muda kidogo, kasema, “Mama, kamwe sikupata nafasi ya kukuuliza ilikuwaje.” Kasema, “Usiku mmoja waliniambia ‘nikae chonjo’, na kesho yake asubuhi, wakasema ulikuwa ‘mzima.’” Kasema, “Kwani da— daktari alitumia dawa gani?”

Kasema, “Mpenzi, daktari hakutumia chochote.”

Akasema, “Vema, ulifanyaje hilo?”

43 Kasema, “Je! unajua mahali ile misheni ndogo ilipo hapa chini kwenye . . . karibu na ule mzingo, pale katikati ya mji?”

“Naam.”

44 Kasema, “Kulikuwako na mama mmoja. Walikuwa na mkutano wa maombi kule chini, usiku mmoja, kwenye misheni hii ndogo, maskini kundi hilo dogo nyenyekevu la watu, na,” kasema, “mmoja wao alivuviwa kuja huku na kuniona. Ndipo wanawake wawili wakaja, nao wakaniuliza kama wangeweza kumleta mchungaji wao huku na—na kuniombea, na kunitia mafuta, na—na,” kasema, “na kuniwekea mikono yao, nipate kuwa mzima.” Kisha kasema, “Unajua, niliwaambia ‘hakika.’ Ndipo wakamleta mchungaji huyo huku, naye akaniwekea mikono yake, na kuomba.” Kisha kasema, “Mpenzi, alilisoma moja kwa moja kutoka kwenye Biblia, Marko mlango wa 16, ilisema, ‘Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.’” Ndipo kasema, “Unajua nini? Kesho yake asubuhi, daktari alikanganyika sana, hakujua la kufanya. Sikuwa na homa yoyote.”

45 “Loo,” akasema, “mama, hukujihusisha na kundi hilo, sivyo?” Kasema, “Unaona,” akasema, “sisi shuleni, tulijifunza kwamba Marko 16, kuanzia kifungu cha 9 na kuendelea, haijavuviwa.”

Akasema, “Utukufu kwa Mungu!”

46 “Mbona,” akasema, “mama, unaanza kutenda kama hao watu.”

47 Akasema, “Nilikuwa tu nikiwazia jambo fulani.” Kasema, “Nimekuwa nikisoma Biblia, kotekote, na ahadi zingine mahali pengine, pia, panapofanana na hapo.” Kisha kasema, “Nilikuwa tu nikiwaza, kama Mungu angeweza kuniponya kwa lile lisilovuviwa, angefanyaje na lile ambalo kweli limevuviwa?” Hiyo ni kweli.

48 Kwangu mimi, yote imevuviwa. Mungu, nipe imani ya kuiamini na kuithibitisha!

49 Sasa tutabadilisha sasa, kwa dakika chache tu, kesi ya mahakamani. Sasa, kumbukeni, tunaingia ndani ya chumba cha mahakama, kumleta Yesu, Mungu, jukwaani hapa, na kumfanyia

kesi ya haki. Yeye angali ni Neno, hata wa leo, (mnaamini hilo?), jinsi tu vile Yeye alivyokuwa ni Neno wakati huo. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

50 Sasa, kesi hii, kilichoisababisha, ni a—ahadi za Neno la Mungu dhidi ya ulimwengu. Sasa fahamu mandhari yake vizuri kabisa la sivyo kamwe hutalipata. Kilichosababisha shtaka hili, ni uvunjaji wa ahadi, "Mungu kutotimiza Neno Lake." Ni kukiuka ahadi. Mnajua ni kitu gani.

51 Sasa, daima tunaona ya kwamba wakili wa mashtaka anapaswa kuiwakilisha serikali, ninaamini hiyo ni kweli, wakili wa mashtaka. Kama kuna mwanasheria anayeketi hapa, ninatumaini nimelipata hili vizuri. Wakili wa mashtaka hana budi kuiwakilisha serikali. Kwa hiyo wakili wa mashtaka katika kesi hii ni ibilisi, akilishtaki Neno la Mungu.

52 Mshtakiwa wa hili Neno, ni Mungu Mwenyewe, kwa kuwa Yeye ni Neno.

Shahidi wa Mshtakiwa, katika kesi hii, ni Roho Mtakatifu.

53 Naye—naye mwendesha mashtaka ana mashahidi fulani hapa alasiri ya leo. Nao mashahidi hawa, mmoja wao, ni Bw. Asiyeamini, anayefuata ni Bw. Mwenye Kushuku, na huyo mwingine ni Bw. Mkosa Subira. Wataletwa jukwaani, na kuapishwa, na kujaribiwa.

54 Sasa mna picha ya jinsi mahakama ilivyo, Mungu ameshtakiwa na ulimwengu, kwa sababu, ati "Yeye halitimizi Neno Lake." Naye wakili wa mashtaka anawakilisha serikali, ambayo inauwakilisha ulimwengu. Naye wakili wa mashtaka ni ibilisi, ambaye hukanusha kwamba Neno ni la kweli.

55 Naye wakili mwendesha mashtaka, kwa ajili ya ushuhuda wake, yeye anawaleta mashahidi watatu dhidi ya Neno la Mungu. Na kuthibitisha jambo hilo, yeye atalithibitisha kwenu, alasiri ya leo, ya kwamba, "Mungu halitimizi Neno Lake, wala hali—halipaswi kuchezewa. Si la kweli kabisa. Halina ukweli wowote."

56 Naye Mshtakiwa ni Mungu, ambaye Ndiye Mwandishi tena ni Neno, kwa ajili ya siku hii, kama siku ile ama siku yoyote ile.

Naye mwendesha mashtaka ana mashahidi wake.

57 Sasa unasema, "Wako wapi wazee wa mahakama?" Ninawazungumzia. Ninyi ndio wazee wa mahakama, na pia ninyi ndinyi hakimu. Sasa kumbukeni jambo hilo, ninyi ni wazee wa mahakama na pia hakimu, kwenye kesi hii. Mimi ni mnenaji tu.

58 Sasa mahakama iko tayari. Sasa kukumbushwa nidhamu kunafanywa na wakili wa mashtaka. Kukumbushwa nidhamu kunafanywa ndani ya chumba cha mahakama, alasiri ya leo, kuleta kesi hii kwenye shi—shindano la kuamua.

59 Sasa watu wengi wamewaambia kwamba, “Neno la Mungu haliaminiki. Huwezi kulitegemea,” na kadhalika, nanyi mmesikia haya yote. Sasa hebu na tulilete kwenye kesi ya kweli. Ni wangapi walio tayari, inua mkono wako na kusema, “Ningependa kusikia; na Yesu Kristo, ambaye ni Neno, afanyiwe kesi ya haki”? Na katika mahakama yetu, alasiri ya leo, tutamfanyia kesi ya haki. Acha tu adui achukue maneno ya adui, na lolote analotaka kusema, nasi tuone kama ni kweli. Hebu na tulichambue na kumfanyia Yesu Kristo, aliye Neno, kesi ya haki alasiri ya leo.

60 Sasa, mahakama inaamrishwa utaratibu, shahidi wa kwanza ambaye mwendesha mashtaka anataka kumleta kizimbani ni . . . kizimbani ni Bw. Asiyeamini. Anasimama kizimbani atoe ushahidi. Sasa kumbukeni, Bw. Asiyeamini. Usiwakose watu hawa sasa, la sivyo utakosa kitu fulani, huenda ukakosa uponyaji wako.

61 Bw. Asiyeamini anakuja kizimbani, kutoa ushahidi. Lalamiko lake ni, kwamba, “Neno lote la ahadi ya Mungu si la kweli. Si la kweli.” Anadai ya kwamba, katika Marko 16, alihudumiwa hiyo—hiyo katika wanaouita mkutano wa Roho Mtakatifu. Naye alikuwa na ugonjwa wa tumbo kwa miaka kadhaa, naye akaenda mahali huo ulipokuwa, wanaouita, “mkutano wa Roho Mtakatifu,” naye alikuwa akiamini ya kwamba ahadi hii ya Marko 16 ilikuwa ni ya kweli. Aliwekewa mikono kulingana na ahadi ya Mungu.

62 Hana neno dhidi ya huyo mhudumu; alilisoma mumo humo kutoka kwa Neno. Yeye hamshtaki mhudumu huyo; yeye anamshtaki Mungu. Kwa sababu, si kosa la mhudumu huyo, mhudumu anasoma tu yale Mungu aliyosema mfanye. Na kweli Mungu alisema, katika Marko 16, “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya.”

63 Naye anasema yeye ni mwaminio, naye alikuja kwenye mkutano kama huo ambapo walikuwa wakihubiri kwamba Marko 16 ni ya kweli. Naye mhudumu, mwenye Ubatizo wa Roho Mtakatifu, alidai ni mwaminio na ni mhudumu aliyetumwa kwa ajili ya kazi hiyo, alimwekea mikono yake. Na hiyo imekuwa ni miezi miwili iliyopita, nalo tumbo lake lingali linauma tu kama lilivyowahi kuuma. Kwa hiyo, yeye anadai ya kwamba Mungu si wa haki, kuweka kitu kama hicho katika Neno, wakati si cha kweli.

Sasa hebu aketi. Alitoa ushahidi.

64 Anayefuata kizimbani ni Bw. Mwenye Kushuku. Anataka kutoa ushuhuda. Bw. Mwenye Kushuku anasema alikuwa akisumbuliwa na—na TB, kwa yapata miaka kumi na mitano. Lakini hakupona kabisa bado, iliendelea kuibuka tu, ika—ikazidi tu kuenea. Angepata nafuu kidogo tu, kisha inaendelea.

Ndipo akasikia mahali fulani mjini ambapo palidhaniwa pana mhubiri mtawa anayehubiri, nao watu walikuwa wakidai kuponywa kulingana na ahadi kutoka kwa Mungu, inayopatikana katika Yakobo 5:14, ambapo katika Neno la Mungu inasema, "Kukiwapo na mtu wa kwenu ambaye hawezi, na awaite wazee wa kanisa; nao wawapake mafuta na kuwaombea; kule kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule, Naye Mungu atawainua."

65 Naye akiwa ni mgonjwa, na ni mwaminio, anaenda kwenye huu mkutano ambapo watu hawa wote wanadai ya kwamba walikuwa wakiponywa na mchungaji huyu mtawa. Basi alihudumiwa, kulingana na Yakobo 5:14. Naye mhudumu huyo akamhudumia kulingana tu na Neno, akampaka mafuta na kumwombea, maombi ambayo mchungaji alisema yalikuwa ni "maombi ya imani," ambayo aliamini. Na hiyo imekuwa ni karibu mwaka mmoja uliopita, wala hajapata nafuu hata kidogo kutokana nayo, kwa hiyo Bw. Mwenye Kushuku anadai ya kwamba Mungu hana haki ya kuweka ahadi kama hiyo katika Biblia halafu ashindwe kusimama nyuma yake.

Sasa, kumbukeni, ninasoma ahadi za Injili yote hapa.

66 Shahidi anayefuata atakuja kizimbani sasa. Mwendesha mashtaka anamwita shahidi wake anayefuata, kabla hajaikamilisha kesi yake. Shahidi wake anayefuata ni Bw. Mkosa Subira.

67 Sasa hizi ni tabia za ulimwengu wa roho zinazoishi ndani ya watu. Mnaona, sasa, huishi.

68 Kwa hiyo Bw. Mkosa Subira anakuja, naye anadai ya kwamba siku moja alikuwa akisoma kwenye Biblia. Hakwenda makanisani, bali alikuwa . . . alikuwa ni mwaminio. Kwa hiyo mmoja wao alimwendea mwinjilisti fulani, na huyo mwingine akaenda kwa mchungaji, naye jamaa huyu alikuwa tu ni mwaminio wa siri aliyekaa nyumbani. Basi akaenda na alikuwa akisoma katika Marko mlango wa 11, kifungu cha 22 na 23; kama unayaandika Maandiko hayo. Ambapo, Yesu Mwenyewe, akidai kwamba Yeye ni Mungu, Imanueli, alitoa tamshi hili kwa midomo Yake Mwenyewe, "Amin, amin, nawaambia, mtu atakayeuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitilie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba ulilosema litatimia, litakuwa lako." Na alisema pia, ya kwamba, "Mwombapo, aminini mtapokea mlichoomba, nanyi mtapewa."

69 Yeye anasema amekuwa kiwete miguuni mwake, kwa karibu miaka ishirini na mitano. Ndipo miaka mitano iliyopita, wakati akiketi chumbani, akijisikia alikuwa akivuviwa kulisoma Neno ambalo anadai aliliamini, na kwa moyo wake wote aliliamini. Ndipo basi akasema, kwa sauti yake mwenyewe, "Ulemavu ulio miguuni mwangu, katika Jina la Yesu Kristo, niondokee,"

akasema. Na hiyo imekuwa ni miaka mitano iliyopita, naye amelemaa tu kama alivyowahi kuwa.

70 Kwa hiyo, basi, Bw. Mkosa Subira anataka kuweka ushuhuda wake dhidi ya Neno kuwa lisiloweza kukosea, anataka kuuweka dhidi ya Biblia kuwa ni Neno lililovuviwa, naye anasema ya kwamba ahadi hii si kweli; ameijaribu, nayo "Haikuwa ni ya kweli." Bw. Mwenye Kushuku alisema aliijaribu, na "Haikuwa ni ya kweli." Bw. Asiyeamini alisema aliijaribu, na "Haikuwa ni ya kweli." Mashahidi hawa wote watatu wanatoa masomo ya Kimaandiko, ahadi za Kimaandiko, na kusema ya kwamba ahadi hii inasema hivi, unaweza kuisoma katika Biblia, nao ni mashahidi ya kwamba "Si Kweli."

71 Kwa hiyo, Biblia inapaswa kutupiliwa mbali; maana, kama sehemu Yake moja, kifungu Chake kimoja hakiwezi kuaminiwa, nisingeweza kuamini sehemu Yake yoyote. Inapaswa kuwa yote ni Kweli, ama hakuna hata moja Yake iliyo Kweli. Mnyororo huwa ni imara tu kadiri kiungo chake kilicho dhaifu kuliko vyote kilivyo. Mnajua ninalomaanisha.

72 Sasa mwendesha mashtaka anakuja kuleta mashtaka na kuikamilisha kesi yake. Anataka kuikamilisha. Sasa angalieni kile anachosema. "Mungu hana haki ya kuweka ahadi za kijinga kama hizo katika Neno Lake, kwa ajili ya watoto Wake wanaoamini kuijaribu imani yao kwazo, kwa kuwa si za kweli." Anao mashahidi hapa, kuthibitisha ya kwamba Neno hili ambalo Mungu ameahidi katika Neno Lake kuwa ni Kweli, anao mashahidi wanaoketi hapa, naye anaweza kuonyesha kwa thibitisho la daktari na kutoa ushahidi, ya kwamba wamekuwa wagonjwa, wamekuwa *hiki*, wamekuwa *kile*. "Nao wameyakubali haya Maandiko ya Kiungu, yanayosemekana yamevuviwa, na kuyajaribu, nayo si ya kweli." Yeye ana mashahidi wa kuthibitisha hilo, kwamba, "Maneno haya si ya kweli, kwa kuwa Yeye alishindwa katika kila moja ya hayo hapo."

73 Sasa, sasa angalia tena. "Naye alishindwa. Mungu alishindwa kuwafanya hawa waaminio, ambao waliliamini Neno Lake, wakalichukua vivyo hivyo hasa, wakapitia kwenye utaratibu, vile vile hasa Yeye alivyosema, halafu Mungu hakusogeza kidole kamwe kufanya lolote kuhusu ahadi Yake; miaka na miaka imepita." Ndipo akasema, "Vipi kama Maandiko hayo mengine, kama vile kubatizwa, 'aaminiye na kubatizwa ataokoka,' halafu hakuna mtu yeyote anayeokolewa? Vipi kuhusu haya Maandiko yaliyoahidi ya kwamba Yeye angerudi? Hakuna moja la hayo lililo sahihi. Kwa sababu, *haya* si ya kweli, na *lile* si la kweli. Ni Kitabu tu cha hadithi za kubuniwa. Nao watu hawa ni waaminio. Hata hivyo, Yeye, Mungu, anaahidi ya kwamba mambo yote yanawezekana kwa waaminio, nao hawa ni waaminio.

74 "Hata hivyo, tena, Yeye anadai kuwa hai baada ya kusulibiwa Kwake. Biblia inasema, ya kwamba, 'Yeye alifufuka katika wafu, na anabaki yeye yule jana, leo, na hata milele.' Wala hakuna mtu aliyemwona Mtu huyu mwenye makovu ya misumari mikononi Mwake, akitembea miongoni mwa kanisa, na kadhalika. Pia Waebrania 13:8 si kweli. Yeye si yeye yule jana, leo, na hata milele, maana kamwe hakuwahi kuwa zaidi ya mwanadamu. Yeye hawezi kuitimiza ahadi Yake. Amethibitisha, kwa mashahidi hawa, Yeye hatimizi ahadi Yake, kwa hiyo Kitabu hicho kinapaswa kutupwa kwenye pipa la takataka na kisahauliwe. Hakuna kitu kama hicho."

75 Sasa, kumbukeni, ninatumia sauti ya mwendesha mashtaka, akiikazia kesi yake. "Vema, Yeye alisema katika Luka 17:30, ambapo alisema, 'Katika siku za mwisho, Mwana wa Adamu atafunuliwa,' Mungu angejifunua Mwenyewe kwa Uzao wa Ibrahimu," kama alivyomsikia mhubiri mlokole akihubiri wakati mmoja na kusema ya kwamba Yeye angejifunua Mwenyewe tena katika wanadamu, akiitwa Mwana wa Adamu.

76 "Ufunuo 10, Yeye anasema ya kwamba alidai mjumbe wa malaika wa mwisho, kulingana na wakati wa kanisa katika Laodikia, ambao ulikuwa uwe vuguvugu, ya kwamba Yesu (ambaye alikuwa ni Neno) angetupwa nje ya kanisa. Yeye alidai ya kwamba katika vipindi hivi vya wakati ya kwamba kulikuwako na mambo ambayo hayakuwa yamefunuliwa wale watengenezaji katika siku za mwanzoni, lakini katika siku za mwisho, ya kwamba, mwishoni, ninii wa malaika wa saba, Ujumbe wa mjumbe wa saba, ya kwamba Maandiko haya yote yangefanywa halisi na kudhihirishwa. Hakuna mtu kama huyo duniani, kamwe hajakuwapo wala hatakuwako," yeye anadai.

77 Yeye anadai ya kwamba, katika hilo, "Mungu anadai katika Biblia Yake, ya kwamba kanisa lingekuwa ni la kawaida na kuondoka mahali pake, ya kwamba katika Malaki 4 Yeye angemtuma tena nabii, ambaye amemtuma tayari, mara mbili, Eliya na Yohana Mbatizaji. Yeye angemtuma nabii kwa . . . naye angekuwa katika nguvu za Eliya. Nayo huduma yake, matendo yake, kila kitu, kingekuwa ni Eliya. Halafu basi katika huduma yake, angewaita watu kutoka kwenye hali hii ya kawaida, wairudie ile Imani halisi ya baba wa kimitume. Wala hakuna kitu kama hicho kinachoendelea.

78 "Naye pia anadai ya kwamba mbingu na nchi zitashindwa, bali Neno Lake halitashindwa kamwe." Naye anasema ana thibitisho hapa, alasiri ya leo, kuonyesha ya kwamba Hilo hushindwa. "Naye huyu Yesu aliyefufuka katika wafu ni nani? Ninyi nyote mmepandisha msisimko katika lundo la saikolojia ya kiakili. Wala hakuna kitu kama hicho; mnategemea tumaini la uongo."

79 Sasa, nafikiri hayo karibu yametosha kwake kusema. Nafikiri ameipitia Biblia nzima. Sasa hebu aketi chini, huyu mwendesha mashtaka. Sasa hebu shahidi wa mwendesha mashtaka aketi chini pia. Wanashuka kutoka kwenye kizimba.

80 Basi jukwaani sasa, tutamwita Shahidi wa Mshtakiwa, Roho Mtakatifu. Yeye anakuja kuzungumza. Ninatumaini mnaona jinsi mwendesha mashtaka ameikazia kesi yake kwa Maandiko. Sasa, Shahidi wa Mshtakiwa, ambaye ni Roho Mtakatifu, anakuja kumtetea Mshtakiwa, Neno. Nafikiri wasingeweza kumpata aliye bora zaidi.

81 Kwanza, Yeye anaitaka mahakama hii ijue, ya kwamba mfasiri wa Neno la Mungu, kwa watu, mwongoza mashtaka, ndiye mfasiri yule yule aliyemfasiria Hawa Neno la Mungu. Anaitaka mahakama ielewe jambo hilo, ya kwamba mfasiri huyo ndiye mfasiri wa Hawa, ambaye husema kila sehemu Yake ilikuwa ni kweli ila Neno moja tu. Naye anawatakeni mjue pia. . . Yeye Ndiye, kumbukeni, aliyeiandika Biblia. Pia anawatakeni mjue, ya kwamba, hapo mwanzo, ya kwamba neno moja mbali na Neno la Mungu, lilisababisha mauti yote na huzuni na maradhi. Naye anawatakeni mjue ya kwamba Mungu pia alisema, katika Neno Lake, kwenye mlango wa mwisho, kama ule wa kwanza, ya kwamba, "Mtu yeyote atakayeondoa chochote kutoka Hapa, au kuweka kitu kingine chochote Kwake, ataondolewa sehemu yake kutoka katika Kitabu cha Uzima." Lazima iwe ni Neno, na Hilo pekee. Anataka mahakama ijue kwamba yule aliyetilia mkazo sana haya yote, ni mfasiri wa Hawa.

82 Yeye anawatakeni hili. . . anaitaka mahakama hii ijue tena, huyo ni, Shahidi wa Mshtakiwa, Yeye anataka kuitazamisha mahakama hii na kuwaonyesha ya kwamba ahadi hizo ni kwa waaminio pekee; si wanaojisingizia imani, wasio na subira, ama wenye kushuku. Inabadilisha picha hiyo sivyo? Ni ninii tu. . . Si kwa wale watu wanaojiita waaminio; ni kwa ajili ya waaminio pekee, sio kwa wale wanaosema wao ni waaminio. Shetani husema yeye ni mwaminio, pia, mwajua. Sio kwa hao. Ni kwa waaminio halisi pekee.

83 Naye huyu Shahidi wa Mshtakiwa anapaswa kujua kama hawa watu ni waaminio ama sivyo, kwa sababu, hata hivyo, Shahidi wa Mshtakiwa ndiye—ndiye mwenye kulihuisha Neno Lenyewe. Yeye anajua kama unaliamini ama huliamini. Yeye Ndiye ametolewa na Mungu, kulifanya litimie. Haleluya! Yeye Ndiye anayethibitisha hilo. Yeye Ndiye anayelifanya litimie. Yeye Ndiye anayejua kama limeanguka mahali pazuri ama la, Huyu Shahidi wa Mshtakiwa wa Neno. Angalieni, anataka kuwahamasisha tena waaminio, Shahidi wa Mshtakiwa anajua kama ndivyo ilivyo ama sivyo, Yeye Ndiye mwenye kulihuisha Neno.

84 Na tena anaitazamisha mahakama hii kwenye Neno la ahadi linaloshukiwa. Yeye hakuweka muda wowote maalum kwa mambo haya kutukia.

85 Mnaona jinsi wanavyoweza kuwasomea Neno vibaya? Sasa jamaa hawa wanaosema, “Hebu nione *hili* likitukia,” mnaona, hata hawalisomi Neno vizuri. Hiyo ni kusema, kama mtu huyo ni mwaminio wa kweli, Yeye angali hakuweka kikomo chochote cha wakati.

86 Pia anaitaka mahakama ikumbuke ya kwamba hili Neno limeandikwa, Naye Yesu Kristo, Neno lililodhihirishwa, alisema, “Neno ni mbegu ambayo mpanzi alipanda.” Na mbegu inaweza tu kujizaa yenyewe, kuzaa ahadi yake, kama imo kwenye ardhi nzuri ambayo itaihuisha hiyo mbegu. Amina. Kidogo tunaibadilisha ke—kesi hii, sivyo? Haina budi kuwa katika mahali panapofaa.

87 Punje ya mbegu inayokaa kwenye dawati hili kamwe haitakuza mavuno. Punje ya—ya mahindi hapa juu, kwenye jiwe la bluu, haitafanya kitu. Punje ya mahindi haina budi kuanguka kwenye udongo uliorutubishwa kwa ajili ya punje hiyo ya mahindi, la sivyo haitakua.

88 Naye Mungu alisema ya kwamba Neno Lake ni mbegu ambayo mpanzi alipanda, nayo haina budi kuanguka kwenye udongo mzuri. Udongo huo ni imani. Ni mbegu, nayo haina budi kuanguka kwenye udongo huu, la sivyo haiwezi kuhuishwa. Kwa maneno mengine, Roho Mtakatifu, Shahidi wa Mshtakiwa hapa, anasema ya kwamba hata hawezi kuijia mpaka itakapoanguka kwenye udongo mzuri. Yeye ndiye mwenye kuihuisha.

Shahidi wa Mshtakiwa anamwita shahidi wake wa kwanza.

89 Nafikiri kama mwongoza mashtaka angeweza kuwaita mashahidi, hapa duniani, wathibitishe kwamba Neno si la kweli, nafikiri Shahidi wa Mshtakiwa ana haki ya kuwaita mashahidi wanaoweza kuthibitisha Hilo ni la kweli. Kwa sababu, swali sasa ni kati ya waaminio na wasioamini, pamoja na Neno, wakati Neno likikua.

90 Shahidi wa Mshtakiwa anataka kuleta kwenye mahakama hii, alasiri ya leo, shahidi wa kwanza, ndiye Nuhu. Nuhu alisema ya kwamba aliishi katika wakati wa kisayansi sana. Nuhu anataka kutoa ushahidi. Naye alisema ya kwamba aliishi katika siku ambapo watu walikuwa wameondoka kwenye miujiza na kadhalika. Ndipo akasikia Neno la Mungu likimwambia ya kwamba Yeye atauangamiza ulimwengu kwa maji, nayo maji yangeshuka kutoka juu. Ingenyesha, ambapo hakukuwa kumenyesha hapo kabla. Lakini anasema ya kwamba Ne—Neno la Mungu, yeye akiwa ni nabii, Neno lilimjia, naye akaanza kuhubiri ya kwamba Neno litatimia, kwa sababu Hilo lilikuwa ni Mungu. Na pia anaitaka mahakama hii ijue ya kwamba Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira,

walimjaribu wakati wote. Lakini kwa kuwa yeye ni nabii, akijua ya kwamba Mungu asingeweza kusema uongo, yeye alilishikilia Neno, haidhuru.

91 Walimjia na kusema, "Sasa, Nuhu," Bw. Asiyeamini akasema, "utathibitishaje kuna mvua yoyote kule juu?"

92 "Sijui iko wapi. Lakini kama Mungu alisema hivyo, hilo—hilo latosha."

"Itanyeshaje wakati hakuna mvua yoyote kule juu?"

"Sijui. Bali Mungu alisema hivyo, na hiyo yatosha."

93 Bw. Mwenye Kushuku akaja karibu na kusema, "Kama ingekuwa ni kitu kama mvua kushuka kule, basi itambidi Yeye kushuka hapa na kuichukua mvua na kuipeleka kule juu. Atafanyaje hilo?"

"Sijui." "Na baada ya mimi kuijenga safina . . . "

94 Kwanza yeye anataka kusema, ya kwamba wakati alipotoa tamshi hili, akiwa ni nabii miongoni mwa watu, kila mtu alimcheka, na kusema, "Sioni mvua yoyote."

95 Vema, wakati alipoanza kuijenga safina, wao walisema, "Labda baada ya safina . . . " Bw.—Bw. Kukosa Subira alijaribu kumwambia, "Labda baada ya safina kujengwa, ndipo mvua itanyesha." Lakini wakati safina ilipokamilika, kungali hakukunyesha.

96 Kamwe haikunyesha kesho yake, haikunyesha juma lililofuata, haikunyesha—kamwe haikunyesha mwezi uliofuata, mwaka uliofuata. Ndipo alipoimaliza safina, kungali hakukunyesha.

97 Ndipo basi akasema, siku moja Sauti ya Mungu ilimrudia ikamwambia ya kwamba ataona ishara ya kimbinguni katika maumbile, ya kwamba ndege na wanyama wataingia ndani ya hii. Ndipo Bw. Asiyeamini akamcheka na kusema, "Imekuwa maskani ya ndege. Yeye alijenga kituo cha ndege, badala yake." Nao wote wakamcheka na kumdhihaki.

Lakini, siku moja, Mungu alinena naye, na kusema, "Ingia ndani ya safina."

98 Ndipo Nuhu akasimama mlangoni na kusema, "Mnapata wito wenu wa mwisho. Ingieni!" Wala hakuna mtu aliyeingia ila familia yake mwenyewe.

99 Kwa hiyo anasema aliingia kwenye safina. Naye akaiambia familia yake ndogo ya kupendeza, sasa, huyu ni nabii Nuhu. "Loo, katika saa nyingine, hapana shaka, mvua itakuwa ikinyesha."

100 Na wakati alipoingia, mlango ulijifunga kimbinguni nyuma yake. Akasema, "Unaona sasa, mpenzi," kwa mkewe, kwa wake za wanawe na wanawe, "tumefungiwa ndani pamoja na Mungu.

101 “Sasa tuna dirisha hapa juu. Panda vipandio upesi, upesi sana. Usiikose. Kwea, upesi sana, upande hapa juu sasa. Kuko karibu kunyesha, hapana shaka.”

102 Na baadhi ya watu huko nje waliomsikia akihubiri, wakasema, “Sijui kama maskini mlokole huyo mzee angeweza kuwa anasema kweli?” Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, Bw. Mkosa Subira, wote walikaribia, wakasema, “Tutaona.” Kasema, “Nuhu uko humo ndani?”

“Naam.”

“Fungua, tungetaka kuangalia humo ndani.”

103 “Mungu amefunga mlango. Siwezi kuufungua. Hakuna komeo humu ndani la kuufungulia.”

104 Sasa wao wakasema, “Maskini mwendawazimu huyo, aliingia mle na kuufunga huo mlango, na kujaribu kutufanya tufikiri . . . Ni udanganyifu. Anajaribu kututisha.”

105 Na hao hapo mashahidi wa mwendesha mashtaka, wameketi pale, wakisikiliza haya yote, kwa kuwa wana hatia ya kulifanya. Biblia ilisema hivyo, “Wenye kudhihaki!”

“Nao wakanidhihaki, wakanifanyia mzaha.

106 “Na hata, mimi mwenyewe, nilikuwa nikiitarajia mvua. Siku nzima, hakukuwako na mvua. Kesho yake, hakukuwako na mvua. Siku iliyofuata, hakukuwako na mvua. Siku nne, hakuna mvua. Siku tano, hakuna mvua. Siku sita, hakuna mvua. Lakini Mungu hakuniambia itanyesha lini, Yeye alisema tu, ‘Itanyesha.’ Yeye hakuweka kipimo chochote cha wakati. Alisema tu, ‘Itanyesha.’”

107 Kamwe hakusema, “Mara mtakapoiweka mikono juu ya wagonjwa, wataruka juu na kukimbia huku na huku sakafuni,” kama vile Mwenye Kushuku anavyowataka mfikirie. Yeye alisema, “Watapata afya.” Kamwe hakusema ni lini, jinsi gani. “Watapata afya!”

108 Akasema, “Maombi ya imani yatamwokoa mgonjwa,” katika Yakobo 5:14, “Mungu atamwinua.” Wakati gani? Yeye hakusema. Alisema tu atamwinua.

109 Marko 16, Yeye alisema, “Ukiuambia mlima huu, ‘ngoka,’ wala usitie shaka moyoni mwako, bali uamini ya kwamba yale umesema yatatimia.” Yeye hakusema ni lini. Alisema ingetukia! Haleluya!

110 Unamwona huyo mfasiri wa uongo wa Neno hapo? Ndipo unasema, “Vema, hebu nikuone ukimfanya mtu *huyu*, amekuwa kwenye kitimaguru muda mrefu. Hebu nilione. Yeye anasema ana imani.” Huyo ibilisi! Mnaona yeye ni nani?

111 Yesu kamwe hakusema wangeruka moja kwa moja juu na kupona hapo hapo. Wapentekoste wengi wamewazia jambo lile lile, lakini Biblia kamwe haikusema hivyo. Yeye alisema,

"Kama wao waliliamini jambo hilo, wangepata afya." Naye anao mashahidi Wake hapa kuthibitisha hilo.

112 Nuhu akasema, "Baada ya miaka mia moja na ishirini, ndipo kukanyesha." Lakini, ilinyesha. Nuhu alijua ataiona katika kizazi chake, kwa sababu aliijenga safina, alikuwa tayari kuingia ndani.

113 Sasa, sasa tunaona ya kwamba hiyo ilikuwa ni kweli. Sasa huyo ni Nuhu, shahidi wa kwanza.

114 Sasa, shahidi wa pili, tutakayemwita. Hebu tumwite Ibrahimu. Yeye alisema, "Nilikuwa nabii, nami nilitabiri chini ya uvuvio wa Mungu. Naye akaniambia ya kwamba mke wangu, akiwa na umri wa miaka sitini na mitano, nami sabini na mitano, kwenye umri huo, kwenye wakati huo, ya kwamba nitampata mtoto kwa Sara. Hata hivyo, hakika, yeye alikuwa . . . Nilikuwa tasa; yeye alikuwa, tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa. Alikuwa amepita wakati wa kukoma hedhi, kwa miaka ishirini, ama zaidi. Nilikuwa nimeishi naye miaka hii yote, na hapakuwapo na ishara yoyote ya watoto. Alikuwa, tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa. Na, lakini Mungu aliniambia nitampata mtoto mchanga kwake.

115 "Nawe wajua, Bw. Asiyeamini, Bw. Mwenye Kushuku, na Bw. Mkosa Subira, baada ya siku ishirini na nane za kwanza, wakati hakuna kitu kilichotukia kwa Sara, walinicheka na kunifanyia mzaha. Mwaka wa kwanza, walinijia na kusema, 'Una watoto wangapi sasa?'"

116 Lakini, baada ya miaka ishirini na mitano, mtoto huyo mchanga akajitokeza. Lilitukia. Mungu hakusema, "Utampata mtoto juma lijalo, kwa Sara." Yeye hakutaja wakati wowote. Yeye alisema angempata mtoto kwa Sara. Kamwe hakusema ni lini. Alisema tu angempata.

117 Kwa hiyo Ibrahimu akasema, "Nami sikusita kwa ahadi hiyo, kwa kutokuamini. Bali kadiri ilivyokawia, ndivyo nilivyozidi kupata nguvu wakati wote. Na nilipoona ninazidi kuwa mnyonge kimwili, ambacho kilikuwa ndicho kizuizi cha kuja kwa mtoto huyo, badala ya kuwa dhaifu zaidi katika imani, nilipata nguvu zaidi katika imani, kwa maana nilijua ya kwamba Mungu aliweza kulitimiza Neno Lake.

118 "Kwa hiyo siku moja nilikuwa nimeketi, nikizungumza na Sara, ndipo Malaika wa Bwana akaja. Watu watatu, wawili wakaenda Sodoma; Mmoja akasimama karibu nami na kuzungumza nami, na kuniambia mambo yatakayotukia. Nami nilikuwa mkongwe na mabega yangu yameinama, naye Sara alitembea kwa shida. Na, mwajua, kesho yake tu, nikaanza kuona hicho kibyongo kikitoweka mgongoni mwangu. Nazo nywele zangu zikaanza kuwa nyeusi, nayo mashavu ya Sara yakawa mekundu."

119 Sasa mnasema, "Ulokole, Ndugu Branham!" Hebu kidogo, angalia kama alifanya hivyo. Angalia, waligeuka wakawa kijana mwanamume na mwanamke. Sasa unasema, "Loo, Ndugu Branham!" Sasa, Mungu huuficha Ujumbe Wake katikati ya mistari. Seminari kamwe haitajua Hilo. Hiyo ni kweli. La, la. Ni hadithi ya mapenzi.

120 Mke wangu pale, huniandikia barua. Naye anasema jambo moja kwenye barua hiyo, bali ninaweza kusoma katikati ya mistari. Ninajua kile anachozungumzia, maana ninampenda, ninajua tu tabia yake. Ninajua kile anachomaanisha, "Nimeketi hapa usiku wa leo, Billy. Watoto wamelala. Ninakuwazia." Loo, na—najua kile anachomaanisha, mnaona, mnaona, maana ninampenda.

121 Na kama unampenda Mungu, na Roho wa Mungu yumo ndani yako, Roho Mtakatifu Mwenyewe Ndiye mfasiri wa hili Neno.

122 Angalieni, walikuwa ni wakongwe sana sasa, Biblia ilisema hivyo. Upesi sasa, tunafika mwisho. Ndipo akasema, "Niligeuka nikawa kijana mwanamume. Yeye akageuka akawa msichana."

Mnasema, "Loo, Ndugu Branham!"

123 Sikilizeni, kusudi wapate mtoto huyo mchanga . . . Tumbo lake la uzazi lilikuwa limekufa; mtiririko wake wa uhai ulikuwa umekufa. Sasa kupata . . . Ingembidi kumfanyia tumbo lingine la uzazi. Ingempasa kufanya hivyo? Halafu hawakuwa na hizi chupa wanazoziingiza mdomoni mwa mtoto mchanga, kusudi mama apate kuzurura kila mahali. Siku hizo, ilibidi anyonyeshwe na mama. Kwa hiyo ili kufanya jambo hilo, vena za maziwa zilikuwa zimekauka, kwa hiyo ingembidi kufanyiza vena mpya za maziwa, na kadhalika, apate kumnyonyesha mtoto. Na jambo lingine, mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja, aingie katika utungu wa kuzaa? Ingembidi amfanyie moyo mpya. Mnaona? Kwa hiyo hakuutia kiraka tu. Yeye alionyesha, ndani yake, kile atakachoufanyia Uzao wote wa Ibrahimu, watageuka kuwa wapya, watapata mwili mpya wapate kumpokea Mwana ajaye ambaye tunamtarajia. Ningali ninaamini ahadi hiyo.

Unasema, "Ulokole!"

124 Vema, hebu kidogo. Angalia, walifanya safari, maili mia tatu kutoka mahali walipokuwa, huko chini kwenye nchi ya Wafilisti, hadi Gerari. Na huko chini kulikuwako na kijana jina lake Abimeleki, yeye alikuwa ni mfalme, naye alikuwa akimtafuta mpenzi, na hao wasichana wote warembo wa Kifilisti. Huyu hapa anakuja maskini bi-kizee, Sara, sasa, amejifunika shali yake, na Ibrahimu. Ndipo Ibrahimu akasema, "Mpenzi, nataka unifadhili." Kasema, "Wewe unaonekana mrembo sana, wakati huyo mfalme atakapokuona, yeye atakuchukua kama mkewe." Na watu walipomwona, yeye alikuwa ni mrembo sana! Bi-kizee?

Yeye alikuwa ni mrembo sana, hata, Abimeleki akamchukua awe mkewe.

125 Ndipo akamtokea Abimeleki katika ndoto, na kusema, "Mume wake ni nabii Wangu. Ukimgusa, uko kama mtu mfu." Hiyo ni kweli?

126 Anaonyesha hapo atakalowafanyia watoto wote wa Ibrahimu. Kasema, "Yeye hakusema wakati angefanya jambo hilo, bali alisema angelifanya." Hilo ni sawa, rafiki, hebu lisonge mbele tu. Atalifanya kwa vyovyote vile. Aliliahidi. Sasa, lakini miaka ishirini na mitano baadaye, Sara alimpata mtoto huyo, kutoka wakati wa ahadi ile. Neno halikusema angempata wakati gani, bali lilisema angempata.

127 Hebu tuharakishe na mashahidi hawa sasa. Shahidi wa tatu, Musa. Alisema Mungu alimpa ishara ya kufanya, kuthibitisha ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno kwa ajili ya wakati huo. Yeye alilichukua Neno, pamoja na ishara na Sauti, naye akashuka akaenda mbele ya Mchungaji Farao. Ndipo Mchungaji Farao akasema, "A-ha, huo ni ujanja rahisi wa kichawi. Ninao watu hapa wanaoweza kufanya jambo lile lile." Nao wakalifanya. Waigaji! Akasema, "Kama nisingalikuwa nabii na kujua ya kwamba hilo lilikuwa ni Neno lililoahidiwa, ningalisema hayo hayafai kitu,' maana hawa waigaji hapa nje wanafanya jambo lile lile ninalofanya." Bali alijua lilitoka kwa Mungu, kwa hiyo akashikilia imara.

128 Mungu alisema angewakomboa watu nao wangekuja kwenye mlima fulani. Alitarajia labda wangerudi siku hiyo. Lakini, ilikuwa ni miaka mingi baadaye, bali walirudi. Walifika mlimani. Mungu akalitimiza Neno Lake. Aliwapeleka kwenye nchi ya ahadi, kama alivyosema. Yeye alikuwa ameamini Neno la Mungu.

129 Sasa upesi sana nitamchukua shahidi mwingine, shahidi wa nne, ni Yoshua. Yeye alisema, "Wakati Mungu alitupa ahadi, nasi tukaenda kwenye. . . " Ni takriban maili arobaini na kitu tu. "Basi tulipofika Kadeshi-barnea, Musa aliwatuma mashahidi waende waone kama tungeweza kuiteka au la. Na, loo, Waamaleki, na hao majitu wakubwa, na kuta ndefu," kasema, "tusingeweza kuiteka, hata kidogo, ilivyoonekana."

130 Lakini mtu fulani alienda kule na akaleta thibitisho kwamba nchi hiyo ilikuwa ni nzuri. Kwa hiyo akasema, "Makabila mengine yote, wao walisema, 'Loo, hatuwezi kuiteka.'" Akasema, "Nilisimama na kuwatuliza watu, na kuwajulisha si ukubwa wa kitu kile huko nje; ilikuwa ni ahadi ya Mungu, Naye Mungu angefanya jambo hilo." Akasema, "Baada ya kuwatuliza watu hao, Yeye hakutuvusha, kesho yake, juma lililofuata. Miaka arobaini baadaye, Yeye alituvusha. Bali hakusema ni lini atatuvusha; Yeye alisema angetuvusha, kwa hiyo tukavuka."

131 Ningetaka Isaya aje kwa dakika moja. Mwangalieni Isaya. Yeye alisema, "Nilikuwa nabii aliyethibitishwa miongoni mwa watu. Kila mtu aliniamini mimi. Kutoka kwa Mfalme Uzia, kwenda chini kabisa, waliniamini. Nilikuwa nabii aliyethibitishwa. Nilichosema, Mungu alikitimiza. Yeye—Yeye aliyafanya maneno yangu, niliyosema, yatimie, kwa kuwa niliyanena katika Jina Lake, Yehova." Akasema, "Siku moja, Yehova alinena nami na kusema, 'Nitawapa ishara, bikira atachukua mimba.' Nami nikafanya hivyo, nililisema tu kama vile Yehova alivyosema."

132 Kasema, "Nami ninawataka mjue ya kwamba, mahakama hii, ya kwamba kila msichana wa Kiebrania aliweka tayari vijiatu na kila kitu ampate mtoto huyu mchanga. Bikira alikuwa atachukua mimba. Na ikaendelea, miezi, halikutukia. Majuma, halikutukia. Kama miaka mia nane baadaye, likatukia, bali bikira kweli alichukua mimba na kumzaa mtoto." Yehova kamwe hakumwambia lingetukia kesho, bikira fulani katika kizazi chako. Yeye alisema tu, "Bikira atachukua mimba," na hilo linatosha. Hakusema ni lini. Alisema tu angechukua.

133 Sasa, kama inaipendeza mahakama, naweza kuwa shahidi wake anayefuata? Ningetaka kumtetea, shahidi anayefuata. Ahadi ya Neno kwa ajili ya siku hii, ndiyo ninayoishuhudia.

134 Wakati wa kuzaliwa, kama mvulana mdogo huko Kentucky, mnaliona kwenye kadi za maombi na kila kitu, ile Nuru ilisimama pale. Niliwaambia mama yangu na baba yangu, kotekote katika wakati. Natumaini hili halisikiki la kibinafsi, bali ninasimama tu kama shahidi mbele Zake. *Hili* ni Yeye katika umbo la Neno. Sikujua lililomaanisha; hakuna mtu aliyejua. Huko nyuma katika hiyo milima, katika ninii ndogo ya kale . . . Hata hatukuwa na dirisha la kioo kama ninyi nyote mlivyo nalo sasa; mlikuwa na maskini kilango kidogo ulichokisukuma ukakifungua kama dirisha. Na asubuhi hiyo, Nuru ikaingia.

135 Ningewaambia watu, nimwambie mama. Mambo ambayo ningemwambia, sikuzote yangetukia jinsi hiyo. Hawakuliamini. Walisema, "Sivyo." Lakini kama miaka thelathini baadaye, Mungu alilithibitisha kwa thibitisho la kisayansi, ya kwamba lilikuwa ndivyo. Lilikuwa ndivyo, maana ni ahadi.

136 Kwenye ule mti, kwenye umri wa miaka saba, ambapo Sauti ilinena nami na kusema, "Kamwe usivute sigara, kutafuna, wala kunywa pombe, au kuutia mwili wako unajisi."

137 Nami nikiwa kwenye nyumba ya wauza pombe haramu, hata sikujua Biblia ilikuwa ni kitu gani, si zaidi ya neno tu. Huenda tungeweza kupata shajara ya mwaka, bali sio Biblia nyumbani mwetu. Si kitu ila lundo la . . . Si kuzungumza dhidi ya watu wangu, lakini Mungu anajua yote kuhusu hayo. Hapakuwapo na njia kamwe, watu wangu kabla yangu, huko nyuma ya hapo walikuwa Katoliki. Wote walikuwa wamefunga ndoa nje ya

kanisa na wakaondoka, na hapakuwapo na dini yoyote hata kidogo. Hata hatukuijali.

138 Lakini Yeye—Yeye aliniambia kile kingetukia, ya kwamba haikunipasa kuvuta sigara, au kunywa pombe, wala kuuchafua mwili wangu kwa njia yoyote, kungekuwako na kazi nitakayofanya nitakapokuwa mtu mzima. Vema, ilikuwa ni miaka na miaka baada ya hapo. Nilijuaje ya kwamba ningekuwa mhudumu? Nilichukia wazo la mhubiri. Lakini ilitendeka, kwa vyovyote vile. Inaonyesha ya kwamba Yeye hulitimiza Neno Lake. Miaka kumi na saba baada ya Yeye kunitokea huko kichakani . . .

139 Tunaona, kesho yake baada ya jambo hilo, Yeye alinionyesha daraja linalovuka mto, kwa mapana, likaonyesha watu kumi na sita wakianguka kutoka humo. Nikamwambia mama. Huku nimeketi kuuegemea mti, nikiiangalia. Kasema, "Ulishikwa na usingizi, mpenzi."

Nikasema, "La, kamwe sikulala, mama. Niliiangalia."

140 Miaka kumi na saba kamili tangu siku hiyo, Daraja la Manispaa huko Jeffersonville lilijengwa kuuunganisha na Kentucky, na wa saba . . . Nao watu kumi na sita wakapoteza maisha yao humo, kama tu vile lilivyosema. Loo, vivyo hivyo Bw. Asiyeamini amenijaribu kotekote!

141 Na hebu nivute nadhari ya huyu mwendesha mashtaka kipofu, kuhusu Yesu kuwa hapa na makovu ya misumari mkononi Mwake. Kamwe hakusema kitu kama hicho. Yeye alisema, wakati atakaporudi kutoka Mbinguni, ya kwamba, "Kila goti linapaswa kupigwa, na kila jicho litamwona, na kila ulimi utakiri." Yeye aliahidi tu kuzirudisha nguvu za Roho na kulithibitisha Neno Lake, la Marko, na kile ambacho angefanya. Yeye haninii tu . . . Ni kwamba tu hawalipati.

142 Sasa, juu ya msingi wa mjadala huu, alasiri ya leo, nasi tukiishi . . . Ambapo, itanibidi kuacha, mnaniona nikigeuza kurasa hizi za fungu la maneno na kadhalika, sina budi kulielezea, lakini ninafikiri tuko karibu sana sasa kulipata.

143 Sasa bado wao hawataamini. Yesu aliahidi ya kwamba, "Kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na kama ilivyokuwa katika siku za Lutu, itakuwa katika siku ya mwisho." Tunalo. Lipo hapa. Tayari limethibitishwa, ni Maandiko mangapi tu! Katika wakati wa Sodoma, kile kilichompata Ibrahimu, kingeurudia tena Uzao wa kifalme wa Ibrahimu, ulio ndani ya Kristo; Kristo akirudi katika umbo la Neno, akitenda kazi katika wanadamu, na akionyesha ishara ambazo aliahidi zingeonekana, zingefanywa. Yeye aliahidi angelifanya. Mungu aliahidi. Naye Mungu atatimiza ahadi Yake.

144 Na sasa, miaka michache iliyopita, niliwaambia ya kwamba alinena nami na kusema, "Kutakuwako na hatua tatu za huduma hii. Na moja ya hizo itakuwa ni kuwashika

watu mkono, nami ningejua shida zao zilikuwa ni nini." Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Hakika. Hivi sikuwaambia, "Kama ningekuwa mwaminifu," ya kwamba Yeye aliniambia, "ingetukia ya kwamba ningejua hata siri zilizokuwa moyoni mwao"? Je! niliwaambia hilo? Ni wangapi wanaokumbuka hilo? Je! lilitukia? Halikutukia kesho yake, ilikuwa ni miaka kadhaa baadaye, bali lilitukia.

145 Naye alinena huko chini mtoni, akasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangaza kuja kwa Kristo, mwishoni mwa huduma yake, Yesu alikuja. Na kama vile Yohana alivyotumwa, vivyo hivyo na huduma yako itakutangulia Kuja kwa Pili kwa Kristo." Na kumekuwako na uamsho wa ulimwenguni kote miongoni mwa watu wa Mungu, kote ulimwenguni, katika miaka kumi na mitano iliyopita; uamsho wa muda mrefu kuliko yote. Mwana historia yeyote anajua ya kwamba hakuna uamsho unaodumu zaidi ya miaka mitatu. Na huu ni miaka kumi na mitano. Na hebu liangalie kanisa leo hii, limepoa kabisa. Tunakungojea Kuja Kwake. Yeye anajithibitisha Mwenyewe, akijionyesha.

146 Sasa, mambo haya yote yametukia. Yeye aliahidi mle ndani, ya kwamba, "Ungezijua siri za moyo."

147 Sasa hatua ya tatu ndiyo kwanza inaibuka katika huduma sasa. Sitachukua wakati kuingia mle, maana nafikiri sipaswi. Lakini wengi wenu hapa mnafahamu jambo hilo, mnaona, yale ambayo yametukia.

148 Sasa, wakati nilipowaambia, wakati nilipokuja kwenye Jiji la Kansas hapa chini kwa mara ya kwanza, na huko chini Arkansas, kwamba mambo haya yangetukia, nayo haya hapa. Sisi ni mashahidi walio hai ya kwamba yametukia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . Mungu amesema yatatimia. Hakusema yatatimia papo hapo. Alisema yangetimia.

149 Marko 16 ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Kama mimi si mwaminio, basi kwa nini Neno hili limethibitishwa kwamba ni Kweli?

150 Kama ninyi si waaminio, basi ni kwa nini Mungu akawapa Roho Mtakatifu? Huenda mkawa na kila namna ya mathibitisho, huenda mkakimbia, mkanena kwa lugha, na mkafanya mambo kama watu walio na Roho Mtakatifu; bali kama hicho si kitu cha halisi moyoni mwako, kamwe hakitalifanya hilo Neno liishi. Bali kama ni kitu fulani cha halisi mle ndani, "mbingu na nchi zitapita, bali hilo Neno haliwezi kushindwa."

151 "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Nanyi mnawaona wengine wakipata afya. Yeye hakusema wangepata afya papo hapo. Alisema, "Wangepata afya kama wakiamini."

152 Ni wangapi wanaosikia, kwamba ni Kweli? Ni wangapi wanaamini ya kwamba Neno la Mungu lingali ni kweli?

Linatafsiriwa tu vibaya kwa watu. Hivi hamwamini hivyo? Limefasiriwa tu vibaya.

153 Sasa, sio huko nyuma katika siku za Luther, sio huko nyuma katika siku za Paulo, sio huko nyuma katika siku za Nuhu na mashahidi hawa wengine, sio miaka kumi na mitano iliyopita wakati nilipowaambia mambo haya yangetukia; bali ni leo hii huku Topeka, Kansas, leo hii, saa hii, dakika hii, hebu na tulialike Neno la Mungu kwenye shindano la kuamua. Yeye aliahidi jambo hili lingetukia katika siku za mwisho.

154 Sasa mnaamini yeye hudumisha Neno Lake? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Yeye hana budi kulitimiza Neno Lake, kusudi apate kuwa ni Mungu. Hana budi kulitimiza. Hana budi kulitimiza Neno Lake.

155 Sasa, hivi Yeye aliahidi, "Kama ilivyokuwa katika siku za—za Sodoma, lingekuwa ni jambo lile lile katika kuja kwake Mwana wa Adamu," ya kwamba ange—angefunuliwa katika siku za mwisho kama alivyofunuliwa kwa Ibrahimu na Uzao wake huko Sodoma? Je! aliahidi hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Luka mlango wa 17, kifungu cha 30, mnaweza kukisoma. Sasa, Yeye aliahidi hilo. Alisema lingetendeka. Yesu alisema Maandiko yote hayana budi kutimizwa, yote aliyoahidi.

156 Je! Yeye aliahidi katika Malaki 4, kile angefanya katika siku hizi za mwisho? Na mara baada ya hapo moto ungetokea, na kumteketeza asiyeamini, nao wenye haki watatembea juu ya majivu ya asiyeamini. Hiyo ni kweli. Vema, tupo papa hapa mlangoni.

157 Sasa, kabla tu yale mafuriko makuu kuingia, yeye aliahidi kitu gani? Kabla tu ya kutokea kwa Nuhu—kwa Nuhu . . . ama Musa akija kuwatoa wana wa Israeli, ni kitu gani kilichotukia? Kabla tu ya kule kuja kwa Yesu, ni kitu gani kilichotukia?

158 Yohana, hatukumleta akatoe ushahidi. Tulikuwa naye hapa chini, bali si kama shahidi, jinsi ambavyo aliitwa atoke kwenye theolojia zote za siku hiyo, aende nyikani, kwa maana alikuwa atambue, alikuwa amtambulishe Masihi.

159 Vema, kama tungalishuka kwenda kwenye shule, kwa baba yake. Tuseme, "Sasa, mimi ni rafiki msiri wa baba yako. Loo, yeye alikuwa ni mzee mashuhuri. Ninampenda. Na ninajua . . . Sasa si Ndugu Jones ndiye yule Masihi? Sasa unajua, Yohana, yeye ndiye."

160 Mnaona, yeye alijitenga. Kwenye umri wa miaka tisa, alienda nyikani, kwa kuwa yeye alikuwa mpenda nyika. Roho ya Eliya ilikuwa juu yake. Nayo Roho ya Eliya; haikuwa ni Eliya, yeye alikuwa ni binadamu; ilikuwa ni Roho ya Mungu ikiwa na hilo Neno katika siku hiyo. Naye akaingia nyikani. Ndipo wakati alipotoka, i—ilimbidi kumtambulisha Kristo, sio mtu mzuri, bali, "Yule utakayemwona Roho akishuka juu yake." Sio ati mtu huyo alikuwa ni mwalimu mzuri zaidi ya wote, sio ati

mtu huyo alikuwa wa thamani kuliko wote nchini siku hiyo, bali, “Yule ambaye Roho Mtakatifu Mwenyewe atamtambulisha kama Neno.” Neno Lenyewe lililitambulisha Neno.

161 Sasa Yeye aliahidi hilo katika siku za mwisho. Yesu angefanya, angekuwa ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

162 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Iweni na imani. Msitie shaka. Amininі.

[Dada mmoja ananena kwa lugha nyingine, halafu anatoa ufasiri. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Bwana ashukuriwe.

163 Vema. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

164 Sasa Yeye aliahidi kujitambulishaje? Katika mwanadamu, mwili wa mwanadamu, kama alivyofanya kwa Ibrahimu, “Wakati Mwana wa Adamu . . . ” Itakuwa ni Mwana wa Adamu, sio—sio—sio—sio Mwana wa Mungu sasa; Mwana wa Mungu katika Mwana wa Adamu. Katika Ezekieli, mlango wa kwanza, kifungu cha pili, Yehova alimwita Ezekieli Mwana wa Adamu, vile vile hasa Yesu alivyojiita Mwenyewe. Mnaelewa hilo, kwa mafundisho ya juma hili. Sasa, mnaona, Mwana wa Adamu ni kitu gani? Ni wa kinabii. Malaki 4 ilikuwa ni nini? Kuwa nabii. Mambo haya yaliyokuwa yatukie katika siku za mwisho ni yapi? Sasa, kamwe Yeye hakusema ni lini. Yeye alisema yangetukia, nayo yakatukia. Sasa, ninyi, kama Yeye angali ni Mwana wa Mungu, Mwana wa Adamu; tayari kufunuliwa katika siku za mwisho kwenye kiti cha enzi cha Daudi, kama Mwana wa Daudi. Mnaona, angalieni, basi kama Yeye . . . Kama hiyo ni kweli, Yeye aliahidi jambo hilo, Yeye anawajibika kwa Neno hilo. Anawajibika kwa Neno hilo.

165 Sasa wewe gusa upindo wa vazi Lake kwa imani yako. Nami nimefanya madai haya. Kama ni ya Mungu, yatatimia; ikiwa si ya Mungu, hayatatimia. Na hilo ndilo tu lililo kweli, uone kama hii ni kweli, kama tuko miongoni mwa waaminio ama hatuko. Sasa huna budi kuwa mwaminio, kama vile tu mimi nilivyo mwaminio. Inakupasa kuamini hili kwamba ni Kweli. Kama unaamini, litatukia. Sasa ombeni, kila mmoja wenu, amini kwa njia yako mwenyewe.

166 Hebu tuanzie upande mmoja, tushikilie tu upande mmoja. Na ninii tu, ninataka upande huu hapa kuegemea ukutani, mahali fulani, amini. Iweni na imani. Msitie shaka. Amininі tu, mseme, “Bwana!”

167 Msiniangalie sasa, mnaona. Mnaweza kuniangalia, lakini, angalieni, acheni imani yenu iangalie zaidi ya hapo. Mnaweza kuniangalia kwa macho ya kimwili, bali mwangalieni Yeye kwa macho yenu ya imani, ya kwamba Yeye ni hilo Neno. Na—Naye ndiyo kwanza abadilishe kinyago Chake, mnaona, kutoka kile

ambacho kisingeweza kuonekana kufikia kile kimetangazwa kabisa, Neno lililofanyika mwili. Iweni na imani.

168 Sasa msisogee sasa. Iweni watulivu sana, wenye kicho. Mnaweza kusogea huku na huko, katika dakika moja; bali mwe watulivu sana, wenye kicho.

169 Sasa, ni, ni kitu gani? Ni karama. Karama si kuchukua, kama upanga, na kwenda, kupiga na kuchoma na kuvuta. Hilo silo. Karama ni kujiondoa tu njiani, kusudi Roho Mtakatifu apate kutenda kazi katika mwili wa mwanadamu. Usijaribu kusema, "Utukufu kwa Mungu, nina karama! Nina karama, haleluya!" Kamwe hutaipata. Laiti ungalijua tu jinsi ya kujiachilia!

170 Ni kama kutia gia. Unaona? Jibadilishe mwenyewe katika imani, kutoka kwenye kutokuamini, ingiza tu gia kidogo upesi huko nyuma, useme, "Vema, kwa namna fulani daima nimekuwa mwenye kushuku, bali kweli, sasa, ninaamini sasa." Sasa angalia kile kinachotukia basi. Fanya tu mara moja uone kile kinachotukia. Omba tu.

171 Nami hujaribu kujiondoa kwenye Ujumbe, kuingia kwenye karama. Karama, kwa, kusudi Neno lipate kujitambulisha kwa—kwa, kama Waebrania 4:12 isemavyo, "Pambanua, tambua siri zilizoko moyoni."

172 Ombea shida yoyote uliyo nayo. Omba, na useme tu, "Mungu, mi—mimi ni mhitaji. Mtu huyo hanifahamu, lakini mimi ni mhitaji."

173 Katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa ajili ya utukufu wa Mungu, na kulingana na Neno la Mungu ambalo ndiyo kwanza nimalize kulihubiri, ninaichukua kila roho hapa ndani chini ya mamlaka yangu.

174 Sasa, haijalishi kile kinachotukia . . . Huenda jambo fulani likatukia katika dakika moja tu. Kuna mkosoaji anayeketi hapa, nami ninafikiri tu jambo fulani liko karibu kutukia. Unaona? Kwa hiyo iweni tu na kicho kabisa. Kama kitu chochote kikivurugwa, wewe keti tu kimya. Wewe keti tu kimya kabisa, acha mtu huyo afanye kile wanachotaka kufanya. Angalieni kile kitakachotukia. Hebu wachukue hatua, na mwone kinachotukia. Mtaona kama Yeye ni Mungu ama siye. Inawapasa kumwona katika vita. Mmemwona katika uponyaji; mwangalieni katika vita. Shetani anajaribu awezavyo kufanya hilo. Lakini ninii tu—mwacheni tu alifanye mara moja, mwone kinachotukia.

175 Kuna mtu mwingine anayeketi hapa ambaye amekuwa akiugua, ameketi papa hapa chini, mtu na mkewe. Mke anaomba. Yeye anamwombea mkewe. Ni ugonjwa wa neva, neva usoni. Yeye kidogo ni mwanamke mnene. Mume wake amevaa shati jeupe. Yeye anamwekea mikono. Hiyo ni kweli. Inua mkono wako, ikiwa hiyo ni kweli, kama hilo ndilo unaloombea. Usijali. Utakoma. Ni ahadi, kama utaamini. Uligusa vazi Lake.

176 Yupo mama anayeketi papa hapa nyuma upande *huu*, anaugua ugonjwa wa wanawake. Ninatumaini ninii yake... Ee Mungu! Bibi Reed, unajua sikujui. Lakini hiyo ni kweli, sivyo? Ulikuwa ukiomba, "Bwana, unirehemu." Amekurehemu. Utakuacha sasa. Amini tu kwa moyo wako wote. Usitilie shaka. Kuwa na imani.

177 Hapa, huyu hapa mama anayeketi papa hapa mwishoni, amevaa kofia ndogo inayoonekana ni nyeusi. Anaomba kuhusu...Ni shida. Ana shida. Hivi hamwoni ile Nuru inayoning'inia juu yake pale? Mnaona? Amekiinamisha kichwa chake. Ana shida ya magoti yake. Aliyaumiza magoti yake. Alianguka na kuyaumiza magoti yake. Mnaona? Simjui; Mungu anajua hilo. Lakini hiyo ni kweli, sivyo, mama?

178 Hapa, weka mkono wako juu ya mama huyo mwingine anayeketi karibu nawe; imekuja moja kwa moja mpaka kwake. Anaugua ugonjwa wa neva. Nao ugonjwa huo wa neva umeninii... Yeye anaumwa na jicho. Na macho hayo yalifanyiwa upasuaji, ambao ulisababisha hilo. Hiyo ni kweli, sivyo? Inua mkono wako. Kama unaweza kuamini!

179 Huyu mama mwingine aliinua mkono wake papo hapo kando yake, kidogo lilimchangamsha sana. Lakini sababu, kama utaninii...Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Iko kwenye vifundo vyako vya miguu. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hiyo*. Vema.

180 Yeye alisema angefanya nini? "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Mnaamini hilo?

181 Huyu hapa mwanaume anayeketi mbele yangu. Anaugua yabisi kavu. Yeye kweli...Sijui kama ataupata ama hataupata. Ni mtu wa kama umri wangu. Yeye huumwa na yabisi kavu. Hatoki hapa. Anatoka kwenye Jiji la Kansas. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya? Unaamini Mungu anaweza kuniambia jina lako ni nani? Bw. Francis. Wewe amini kwa moyo wako wote. Yeye alikuwa akijaribu kukunyang'anya huo, bwana. Na yeye—yeye...Ulikuwa ukifikiri nilikuwa nikimaanisha mtu mwingine, bali ilikuwa ni wewe. Ndipo wakati niliposema hilo, hisi ya ajabu kweli ilikuja juu yako, tamu sana na motomoto. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna *hii*.

182 Pia, mke wako anayeketi hapo, yeye ni Bibi Francis. Yeye pia huugua yabisi kavu. Pia ana shida ya macho yake, na shida na masikio yake. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli.

183 Mama anayeketi karibu na yeye, papo hapo karibu na yeye hapo, anaumwa na vena zilizovimba. Kweli. Ana kasoro fulani ndani, namna fulani ya...Ni ugonjwa wa kibofu. Ana ugonjwa wa kibofu. Yeye pia ametoka kwenye Jiji la Kansas. Bibi Gregg. Hiyo ni kweli.

184 Kama mimi sifahamiani kabisa nanyi watu, inueni mikono yenu namna *hiyo*, ili kwamba, ninamaanisha, kwa hawa watu hapa walioitwa, inueni mikono yenu, ninyi watu ambao mmeitwa sasa hivi, kama hatufahamiani.

185 Ni kitu gani? Mungu yule yule aliyeshuka katika mwili wa binadamu, na akala nyama na kunywa maziwa. Naye Yesu alisema . . . Naye Ibrahimu alisema, hasa, ya kwamba Yeye alikuwa ni "Elohimu," Mungu aliyedhihirishwa katika mwili. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku hiyo, ambapo Yehova, Mwana wa Adamu tena, katika mfano wa kinabii, kama alivyokuwa, angerudi tena katika siku za mwisho," kabla tu miili yenu haijabadilishwa. Sisi, sisi tusingeninii . . . Mnaona, Sara asingeweza kumpokea mtoto huyo katika mwili huo, sivyo? Ibrahimu asingeweza, katika mwili wake. Ilibidi mwili wake ubadilishwe. Vivyo hivyo na yetu, ipate kumpokea yule Mwana. Lichukue Neno, Naye ni Mwana. Ni Neno. Mnaamini hilo?

Sasa inamisheni vichwa vyenu kwa dakika moja.

186 Kabisa, kwa moyo wako wote, je! Mungu ana haki ya kutoa ahadi hizi? Unaamini Neno Lake ni la Kweli? Unaamini ya kwamba mashahidi hawa ni mashahidi tu wa uongo, ya kwamba hao hawakuwa na imani ya kuamini hapo mwanzo? Ninyi ndinyi wazee wa mahakamani na ninyi ndio hakimu. Kila wazee wa mahakama hawana budi kuamua, hakimu hana budi kutoa hukumu. Hivi umeamua ya kwamba Neno la Mungu, la Marko 16, ni Kweli? Kama umeamua, inua mkono wako. Nimewaleta mashahidi jukwaani, wanaokuja kwa njia ile ile kama hii katika siku za mwisho, na kuthibitisha ya kwamba Neno la Mungu lilikuwa ni la kweli. Nalo Neno la Mungu linaahidi jambo hili katika siku za mwisho. Nami nipo hapa, nanyi mpo hapa, mbele zenu, kuthibitisha hayo mengine, kila mmoja wenu. Kila mmoja wenu angeweza kuitwa, mmoja mmoja, namna hiyo, kama mnaamini. Waulizeni hawa watu, zungumzeni nao, ambapo Roho Mtakatifu ameita.

187 "Unafanya nini sasa, Ndugu Branham?" Ninajaribu kuondoka Kwake. Linaendelea kutendeka kila mahali jengoni; unaiona tu ikimulika.

188 Mnaona, kwa jambo hilo, ninajaribu kuwafanya mliamini. Iweni na imani na Mungu. Aminini hilo. Yeye ana haki ya kuandika hili. Amelithibitisha, na kulithibitisha kwamba ni la Kweli. Yeye alilitabiri, miaka thelathini iliyopita, na kulithibitisha leo hii. Alilisema, miaka elfu mbili iliyopita, na kulithibitisha leo hii. Neno Lake ni Kweli. Na kila Neno la Mungu lina pumzi, na lote ni Kweli. Nayo Marko 16 ilisema, "Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa nao watapata afya."

189 Wazee wa mahakama, uamuzi wenu katika mahakama hii ni nini alasiri hii? Je! Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele? Inua mkono wako. [Kusanyiko linasema, "Amina."—

Mh.] Je! mmeshawishika kabisa ya kwamba Marko 16 ni Kweli, Neno la Yesu Kristo, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya"? Inueni mikono yenu. ["Amina."]

190 Basi, Shetani, huna budi kuondoka. Bw. Asiyeamini, huna shughuli miongoni mwetu tena. Bw. Mwenye Kushuku, ama Bw. Mkosa Subira, sijali itachukua muda gani, itatukia.

191 Hivi mnaniita mwaminio? Inua mkono wako kama unaniita hivyo. Mimi ni mwaminio. Nitawaombea, nitaweka mikono juu yenu. Je! mnaamini ya kwamba wachungaji wenu hapa ni waaminio? Inueni mikono yenu. Ni wahudumu wangapi wanaoamini walio huko? Inueni mikono yenu.

192 Nitawaomba wahudumu wanaoamini waje hapa kwa dakika moja. Hilo ni sawa, mchungaji? Kamilifu. Ninamtaka kila mhudumu kwenye jengo hili, ambaye ni mwaminio, aje hapa na kusimama pamoja nami kwa kitambo kidogo. Ninawataka waaminio halisi sasa. Kumbukeni, hatuwataki wanaojifanya waaminio. Tunawataka waaminio halisi. Njoni hapa msimame jukwaani. Mtaona jambo fulani likitukia sasa. "Ninaamini uliniambia Kweli."

193 Sasa kumbukeni, tulieni kabisa kwa dakika moja, wakati wahudumu hawa wakija, ninataka kuwaambia jambo fulani. Sasa ni kitu gani, ni kitu gani kitakachotukia? Tendo lako, kutokana na tendo lako . . . Mtu fulani aliteleza. Ni sawa. Tendo lako, tangu hapa na kuendelea, litakuwa ndio uamuzi wako. Ni wangapi wanaoamini hilo, inua mkono wako.

194 Sasa kila mtu aliye na—aliye na—na kadi ya maombi, simama upande wa mkono wa kulia hapa, njoo upande *huu*. Wewe, kila mmoja wenu kwenye marefu yenu, simama upande wa mkono wa kulia wa marefu yenu, upande wa mkono wa kulia wa marefu yenu.

195 Sasa hao walio kwenye mwisho huo mwingine hapo, itawabidi waje *huku*. Vema.

196 Hawa wote upande *huu*, walio na kadi za maombi, simameni kwenye marefu *haya*; namna hii, kwenye upande wa mkono wa kulia. Huo ungekuwa ni upande wa mkono wa kushoto. Samahani. Upande *huu* huku ungekuwa ndio upande wa mkono wenu wa kulia. Huo ni upande wa mkono wenu wa kushoto. Sasa zungukeni moja kwa moja namna hiyo, mpange mstari wenu.

197 Sasa ninyi nyote wahudumu njoni hapa na mfanye mistari miwili, moja kwa moja kuambaa huku; mistari miwili moja kwa moja kuja huku juu; moja kwa moja kufikia *hapa* kisha mzunguke moja kwa moja *hapa*, kila mmoja wenu.

198 Sasa ni wangapi wenu wanaoamini? Inua mkono wako, useme, "Sasa tena ninataka kumwonyesha Mungu ya kwamba kabisa ninaamini ya kwamba Marko 16 ni Kweli," inua mkono wako. "Sasa ninalikubali."

199 Ni wangapi huko nje ambao hawatakuwa kwenye mstari wa maombi, watakaokuwa wakiwaombea hawa walio kwenye mstari wa maombi, na kundi lote la sisi kwa pamoja litakuwa likiomba kama waaminio? Inua mkono wako.

Sasa na tuombe.

200 Bwana Yesu, Wewe ni Mungu. Wewe ni "MIMI NIKO," aliye mkuu, sio "Nilikuwa," ama "Nitakuwa." Wewe ni "MIMI NIKO," wakati uliopo. Hakuna nguvu zinazoweza kukuzuia. Wewe ni Mungu, wala hakuna aliye kama Wewe. Unayafanya Maneno Yako kuthibitishwa. Umeyathibitisha kwetu, kupitia mashahidi hao alasiri ya leo katika kesi hii; hawa wazee wa mahakama, na pia mahakama hii, na mahakimu watakaokuwako.

201 Tumefanya kesi, ya haki. Tumechukua yale adui aliyosema. Tumechukua yale mwongoza mashtaka aliyosema. Tumechukua yale mashahidi wake waliyosema. Tuliyarudisha pamoja na ushahidi wa Shahidi wa Mshtakiwa, naye amethibitisha ya kwamba Mungu ana haki ya kutoa matamshi haya, kwa sababu yeye huyatimiza, kwa mwaminio, kwa mashahidi wengi zaidi kuliko asiyeamini anavyoweza kutoa mashahidi. Sasa tunajua hiyo ni kweli. Inategemea tu kama watu wamelipata kuwa ni kweli, Neno la Mungu kuwa ni Kweli.

202 Tujalie, Bwana, kwamba kila mtu anayepitia kwenye mistari hii hapa. . .Baba, watu hawa waliosimama hapa. Baada ya mimi kuondoka, huenda mtu fulani akasema Ndugu Branham aliwawekea mikono, bali ninataka watu wajue ya kwamba wachungaji hawa wana haki ya kuwawekea mikono wagonjwa kadiri mtu mwingine yeyote alivyo nayo. Si lazima wangojee mpaka mwinjilisti wa wakati maalum anapopitia hapa, bali mchungaji wao wenyewe ana haki ya kuwawekea mikono. Mungu, jalia kwamba, kila mtu atakayepitia kwenye mstari huu wa mikono hapa leo hii; ambao wameitwa na kuchaguliwa na Mungu, kuwawekea wagonjwa mikono.

203 Tunajua hatuna mikono mitakatifu, bali hatujiangalii wenyewe. Tunaiangalia dhabihu yetu, Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele, Ambaye anatokwa damu mbele ya kiti cha enzi cha Mungu sasa, apate kutusafisha, kulitekeleza agizo Lake. Tujalie, Bwana, ya kwamba kila mwanamume, mwanamke, mvulana, ama msichana, anayepitia hapa, ataondoka kwenye jukwaa hili, akishangilia, vile vile tu kama walikuwa ni wazima na wamepata nafuu na wenye nguvu. Tujalie. Jalia maamuzi ya wazee hawa wa mahakama, wanayodai yalikuwa, Yeye alihesabiwa haki, na jalia sasa hukumu watakayoitoa iwe ndiyo matendo yao tangu sasa. Tusaidie, Mungu, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

204 Ndugu Roy Borders ama mwongoza nyimbo fulani, kama utakuja hapa kwa muda mfupi na kuongoza. Sasa huku macho yenu yamefumbwa.

205 Sasa ingieni moja kwa moja mstarini, wakati mstari wenu ukija. Pitieni hapa. Tuliomba, kila mmoja wa watu hawa. Sababu ya mimi kuwaweka hapa juu, ilikuwa ni hii. Sasa ninyi upande *huu* mtashuka *hivi* na mwingie moja kwa moja mstarini pamoja na hawa, pamoja na hawa hapa, wanapotoka, mnaona. Vema. Sasa ngojeni tu mpaka wao. . . Ngojeni mpaka watakapoondoka. Ngojeni mpaka mstari *huu* utakapotoka; halafu wewe, mama. Papa hapa, dada, ngojea papo hapo. Unaona, ngojea papo hapo, unaona. Mabawabu, baadhi yenu wasaidieni pale, mnaona. Mnaona, hamna budi kuachilia mistari *hii* itoke, mistari *hii* itoke, ndipo mstari *huu* uifuate, mnaona, ikipita.

206 Sasa kama unapitia hapa ukidhania tu, ukibahatisha tu, ondoka mstarini; huenda ikakufanya mgonjwa zaidi. Lakini kama ukipitia hapa, ukiamini, hakuna kitu kitakachouondoa kwako. Ni wangapi wanaojua kwamba kutoka kwenye huu, huu ndio wakati wa kuamua? Ninyi mlio mstarini, semeni, "Hili ndilo. Ninaliamini. Hakuna cha kunung'unika tena kulihusu. Imekwisha, sasa hivi. Nimelikubali Neno la Mungu." Kama hulikubali, usije mstarini, sasa. Amini kwa moyo wako wote, ndipo uje.

207 Mungu amejithibitisha Mwenyewe kwa Neno, na kwa shahidi na shtaka, yupo sasa hivi, "yeye yule jana, leo, na hata milele." Hakuna kilichosalia ila kuweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya. Hawa hapa wachungaji wenu. Mnajua wao ni waaminio. Wao ni wachungaji wenu.

208 Nami siwataki mfikirie kwamba mimi, Oral Roberts, ama mtu mwingine, ndiye tu amechaguliwa kufanya jambo hili. Kila mhudumu amechaguliwa kulifanya. Kila mwaminio, kama ni mhudumu, ama si mhudumu, amechaguliwa kulifanya. Kila mtu aaminiye, ana haki kuwawekea mikono wagonjwa, nao watapona.

209 Sisemi mchungaji wako ama mtu yeyote yule angeichukua karama ya utambuzi. Si lazima wafanye hivyo; huo sio wito wao. Huo sio wito wao, kufanya hilo. Hiyo itakuwa mtu mmoja kwa wakati mmoja.

210 Lakini—lakini tunaona, ya kwamba umeitwa, kama mwaminio. "Ishara hizi zitafuatana na *hao,*" halimwelekezei mtu yeyote, "hao waaminio." Amini hilo kwa moyo wako wote sasa.

211 Ndugu Roy, uongoze ule wimbo, *Amini Tu*. Kila mtu katika maombi. Wahudumu, wanapopita hapa, wawekeeni mikono. Nanyi walei na marafiki, mnapopitia hapa, msiwe na shaka hata moja niani mwenu; pitieni tu moja kwa moja mstarini, mkitokea hapa, mseme, "Imekwisha."

212 Sasa kumbuka, umekuwa mzee wa mahakama katika kesi hii. Uliinua mkono wako ya kwamba umetoa uamuzi wako.

Kila mtu anayeelewa, aseme, “amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Umetoa uamuzi wako. Sasa utakalofanya tangu sasa litathibitisha kama ulisema kweli au la. Hu—hukumu yako itapitishwa kwa yale ufanyayo tangu sasa. Hiyo itakuwa. Utakuwa hakimu na mzee wa mahakama. Kama kweli unaamini hilo, halina budi kutukia. Kama unajifanya mwaminio, halitatukia.

213 Maana, imethibitishwa na Neno, kwa Uwepo wa Mungu, kwa kila kitu kilichopo. Kuna jambo lolote lililosalia kufanywa? Kama Yeye angekuja moja kwa moja hapa, alasiri ya leo, je! angeweza kukuponya? La, la. Yeye amefanya hivyo tayari. Unaona? Yeye kabisa. . .Hakuna kitu kilichosalia kufanywa sasa. Yeye amejithibitisha hapa, kwa Neno, akathibitisha kila kitu. Jambo pekee likupasalo kufanya. . .Umeamua, umesikiza kesi, umetoa uamuzi, sasa njoo ukaonyeshe hukumu yako. Amina. Mungu awabariki.

214 Vema. [Ndugu Borders anaanza kuongoza kusanyiko katika kuimba *Amini Tu*—Mh.]

215 Iweni katika maombi sasa, ndugu. Na hebu kila mmoja wa mabawabu awapishe watu. Simameni karibukaribu zaidi sasa. Kila mtu na amguse mtoto huyo, gusa kila mtu. Kila mtu awaguse hao watu, kwa imani sasa. Yafungeni macho yenu. [Ndugu Branham na wahudumu wanaomba na kuweka mikono yao juu ya watu hao. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

> Amini tu,
> Yote yawezekana, amini tu;
> Amini tu, amini tu,
> Yote yawezekana, amini tu.

216 Sasa mnaweza kuuimba hivi, “Sasa naamini, sasa hivi naliamini”? Umeamini? Inua mkono wako, useme, “Kweli ninaliamini.” “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio!”

> Yote yawezekana, sasa naamini;
> Loo, sasa naamini, sasa naamini,
> Yote yawezekana, sasa naamini.

217 Wakati fulani uliopita, kama miaka kumi na mitano iliyopita, ninakumbuka usiku mmoja nikiitwa hospitalini, kwa mvulana aliyekuwa akifa kwa dondakoo nyeusi. Kulikuwako na. . .moyo ulikuwa umemharibikia. Naye baba yake akaendelea kuja mkutanoni, ku—kuniita nikamwombee mvulana huyo. Naye mvulana huyo alikuwa na umri wa kama miaka kumi na tano, kumi na sita. Nami nilikuwa na shughuli nyingi sana, nisingeweza kwenda. Basi hatimaye. . .Kama—kama—kama—kama ukilipeleka kwa mmoja, na huyo mwingine pia, mwajua. Kwa hiyo baba akaendela tu kushikilia, akingojea mpaka wakati huo utakapotimia. Hatimaye, usiku mmoja baada ya ibada, nilienda hospitalini. Vema, daktari akaniambia ya kwamba nisingeweza kuingia ndani. Akasema, “Kwa sababu,

m—mvulana huyo ana dondakoo, nawe ni mtu aliyeoa wala huwezi kuingia na kukichukua kijidudu hicho."

218 Vema, nikamuuliza, "Naomba tafadhali uniruhusu tu niingie." Mtu huyo alikuwa ni Mkatoliki. Nami nikasema, nikasema, "Hivi wewe ni Mkristo?"

Akasema, "Mimi ni Mkatoliki."

219 Nikasema, "Kama kasisi alikuwa amesimama hapa akijaribu kuleta—kuleta kaida za mwisho za kanisa kwa mvulana huyu, je! ungekubali?"

220 Akasema, "Hilo ni tofauti. Huyo ni kasisi. Wewe ni mtu aliyeoa."

Nikasema, "Vipi kama nikitia sahihi karatasi, nijitwike jukumu lote?"

Akasema, "Siwezi kufanya hivyo, bwana."

221 Ndipo nikasema, "Tafadhali." Nikasema hili, "Mimi kwa watu hawa ni kadiri kasisi alivyo kwako."

222 Hatimaye, akanivalisha kama Ku Klux Klan, na vitu hivyo vyote vyeupe, kisha akaniingiza ndani, nami nikamwendea mvulana huyo. Alikuwa amepoteza fahamu, siku mbili ama tatu. Moyo wake ulikuwa ukipiga kwa shida. Nimesahau upumuaji ulikuwa vipi; mdogo sana, ukipiga, kwa shida sana. Nao maskini baba na mama walikuwa wamesimama pale.

223 Ndipo nikapiga tu magoti, na maskini maombi mafupi tu rahisi, nikamwekea mikono, nikasema, "Bwana Yesu. . . " Nilitumia Andiko hili. "Wewe ulisema, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.' Hawa hapa baba na mama, wasingekuwa waking'ang'ania na kushikilia kwamba nimwekee mikono huyo mvulana kama haikuwa kwamba waliamini. Na, Bwana, nisingekuja hapa kama dhihaka. Ninaamini ya kwamba yale nimesema na kufundisha ni Kweli." Kisha nikasema, "Ninambariki mvulana huyu mdogo, katika Jina la Yesu Kristo; jalia aishi."

224 Ndipo wakati niliposimama, maskini huyo mama na baba wakaanza kukumbatiana, na kusema, "Hii si ni ajabu, mama! Si ni ajabu!" Mvulana huyo hakuwa amebadilika hata kidogo; alilala tu pale. Na mimi—mimi nikawaangalia.

225 Naye maskini yule nesi amesimama pale, alikuwa nesi maalum, aliyefuzu chuo kikuu, naye alikuwa pale akimwangalia mvulana huyo. Naye akamwambia huyo mama, akasema, "Mnawezaje kutenda hivyo, huku mkijua mvulana wenu anakufa?"

226 Naye maskini baba huyo, kana kwamba alikuwa na umri wa, loo, nakisia, alikuwa na miaka hamsini na minane, sitini, akaweka mikono yake juu ya mabega yake, kama baba mzee

angalifanya. Akasema, "Mwanangu," akasema, "huyo mvulana hafi," akasema.

227 "Bwana," kasema, sijui hii ilikuwa ni nini, namna fulani ya kadiogramu ama chochote kile, kasema, "upumuaji wa—wake umeshuka sana, na kwa ugonjwa huu, haijulikani katika historia, kama kamwe ukifikia katika hali hiyo, kupata kurudi tena."

228 Ndipo maskini mzee huyo akayapangusa macho yake, akamwangalia. Kamwe sitasahau jambo hili. Akasema, "Kipenzi, wewe unaangalia kwenye chati. Hiyo ndiyo umefunzwa kuangalia. Mimi ninaangalia ahadi aliyoifanya Mungu. 'Wakiweka mikono juu ya wagonjwa, watapata afya.'" Mvulana huyo ameoa na ana watoto watatu, mmishenari huko Afrika. Inategemea kile unachoangalia.

229 Sasa huenda kukawa na wengine hapa, waliokuja hapa, ambao hawakupata kadi ya maombi. Nilimuuliza mwanangu pale chini. Akasema, "Hapana shaka kuna wengi sana huko nyuma, baba, ambao hawakupata kadi ya maombi."

230 Ni waaminio wangapi walio hapa basi? Inueni mikono yenu. Naomba mfanye hivi wakati tukiimba. "Sasa naamini"? Sasa Mungu alikuwa ni mwema kwako. Hivi huwezi, kama mwaminio. . .Haileti tofauti yoyote ni mikono ya nani, mradi tu ni mwaminio. Unaona? Hivi mwaweza kuwekeana mikono, nasi tutaimba wimbo huu pamoja, "Sasa naamini." Na mpaka nitakapokutana nanyi, Mungu awe pamoja nanyi!

> Sasa naamini,

Hiyo ni kweli, weka mikono yako juu ya mtu aliye karibu nawe.

> Sasa naamini,
> Yote (haidhuru ni nini kibaya, mambo yote yanawezekana) yanaweze-. . .(Katika Jina la Yesu, wabariki hawa.)
> Sasa naamini, loo, sasa. . .("Sasa sichezi. La, hii, sasa naamini.")
> Yote yawezekana, loo, sasa naamini.

231 Sasa wote wanaoliamini, inueni mikono yenu namna *hii*, "Ninaliamini sasa." Mungu awabariki.

> Hata tuonane!. . .tuonane!
> Hata tuonane miguuni pa Yesu; hata tuonane!
> Hata tuonane; hata tuonane!
> Mungu awe nanyi hata tuonane tena!

Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa.

> Hata tu-. . .

232 Mungu awe pamoja nanyi, hakika, ayapige mawimbi ya mauti yanayotisha mbele yenu, awapeleke kutoka ushindi hadi

ushindi. Siku moja, miili yetu na ibadilishwe na ifanywe kama mwili Wake Mwenyewe wenye utukufu, ambapo hatutawaombea wagonjwa tena. Mpaka wakati huo, Mungu na awe pamoja nanyi, hata tutakapokutana. [Ndugu Branham anavumisha—Mh.]

Hata tuonane!
Mungu awe nanyi hata tuonane tena!

233 Sasa hebu na tuviinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi ya kufunga. Ni nani atakayeomba? [Mtu fulani anasema, "Ndugu Gibson. Ndugu Gibson."—Mh.] Ndugu Gibson sasa, wakati tukiinamisha vichwa vyetu.

KESI SWA64-0621
(The Trial)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 21 Juni, 1964, katika Ukumbi wa Manispaa huko Topeka, Kansas, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2017 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org